# Nipashe

Jumanne Februari 20, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581592

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**MJANE** wa 'nyama ya swala' apatiwa mtaji wa biashara

UKURASA 3



**ASKOFU** Bagonza aja na tafakuri kifo cha Lowassa

UKURASA 4

**LHRC** yasema mgawo umeme unaminya haki za binadamu

UKURASA 7



**PSG YAJIANDAA KUMTWAA OSIMHEN**

UKURASA 22

## SHERIA MPYA

# Mafao kutumika dhamana mkopo

**NI** kabla mwanachama hajafikia umri wa kustaafu... *Endelea ukurasa 5*

1. Wanaopata ulemavu kupewa mafao maalum
2. Aliyeajiriwa sehemu mbili kuchangiwa kote
3. Wanaoendelea hadi miaka 70 waundiwa utaratibu wao
4. Mafao wategemezi wa marehemu kuongezwa



Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, akikabidhi Tuzo ya Heshima kutoka Benki ya CRDB kwa Mwandishi wa Habari, Eda Sanga, ikiwa sehemu ya kutambua mchango wake katika tasnia ya habari wakati wa semina maalum kwa wadau wa sekta ya habari za uchumi iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. Wengine kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa benki hiyo, Bruce Mwile na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo, Tully Esther Mwambapa.**Habari Uk. 5.**
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 24

## GAMONDI AIFUNGIA KAZI CR BELOUIZDAD

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika hatua ya makundi ya...

## Maandamano ya CHADEMA jijini Mbeya yaiva

UKURASA 16

## BoT: Kuna watu wameficha dola

UKURASA 8

**MICHEZO** SIMBA NA HESABU KALI IKIIFUATA ASEC UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Baba atoa ushahidi kortini kuhusu kifo cha mwanawe

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Lumumbu Mtui anayejihusisha na usafirishaji mizigo na umiliki wa maroli, amedai mahakamani kuwa alipokea ujumbe kutoka kwenye simu ya marehemu mtoto wake, Jonson Mtui kwamba kutokana na kiburi cha mwanawe, kimemponza na aanzie Chalinze.

Alidai kuwa ujumbe ulimfanya apige simu kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Kondoa kuhusiana na ujumbe huo, akimweleza kuwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Chalinze anadai wamekuta gari porini na ndani kuna mwili wa Jonson Mtui na mwili wake wakati huo ulikuwa umehifadhiwa katika Hospitali ya Mlandizi.

Mtui alidai hayo jana katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Jaji Hussein Mtembwa.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Ditrick Mapunda, shahidi huyo alidai mtoto wake alikuwa anaendesha gari aina ya Scania na walikuwa wanafanya kazi ya kusafirisha mizigo.

Alidai kuwa Aprili 29, 2020, akiwa nyumbani kwake Kondoa, alifika mtoto wake Jonson akiwa pamoja na tandiboi wake, Edward Nyagawa na kumwambia kwamba wamepata mzigo wa mbao Mafinga, wanakwenda kupakia na kupeleka Dar es Salaam.

Shahidi huyo alidai kuwa aliwaruhusu kwenda kupakia mzigo huo na alikuwa anawasiliana nao kujua kama wamefika, alikuwa anawasaliana na Jonson na muda ambao alikuwa hampati, alimpigia tandiboi wake Edward.

Mtui alidai kuwa Mei 21, 2020, alimpigigia simu Jonson ili ampe mzigo wa saruji kutoka Dar es Salaam warudi nao Kondoa, simu hazikupokewa ikiwamo ya tandiboi wake ambayo iliita pasi na kupokewa.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya muda, alipokea ujumbe ukisema “kutokana na kiburi cha mwanao si kiburi kutenda, mwanao kiburi kimemponza, anza na Chalinze”. Ujumbe huo ulitumwa kupitia namba ya simu ya mwanawe.

“Nilikwenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi Kondoa, nilionesha ujumbe, Mkuu wa Kituo kule Kondoa, alipiga simu Kituo cha Polisi Chalinze, baadaye akamwambia kuwa wamekuta gari porini na ndani kuna mwili wa Jonson Mtuli na mwili wake ulikuwa umehifadhiwa Hospitali ya Mlandizi.

Mtui alidai aliwasiliana na vijana wake wa Dar es Salaam, akiwamo Allen Mtui, wafuatilie mwili na baada ya kuupata ulipelekwa Moshi kwa ajili ya maandalizi ya mazishi.

“Huyo tandiboi siku hiyo hakupokea simu yangu, kwenye mazishi hakukanyaga hadi leo (jana) hii nimesimama hapa mahakamani ndipo ninamwona, yule pale, ninaamini yeye ndiye amehusika na kifo cha mwanangu,” alidai.

Daktari Sudi Msakamali kutoka Hospitali ya Msiga, alidai alifanya uchunguzi wa mwili wa Jonson, kipindi hicho alikuwa anafanya kazi Kituo cha Afya Chalinze kama Daktari Mfawidhi.

Alidai kuwa Mei 21, 2020, alifuatwa na polisi kituoni huko kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mwili huo. Baada ya uchunguzi alibaini kifo cha Jonson kilisababishwa na kuvuja damu nyingi.

Pia alidai mwili huo ulikuwa na majeraha kichwani, sehemu ya nyuma na katika paji la uso lenye upana na urefu unaokadiriwa sentimeta 3.3 kichwani.

# Kauli ya Prof. Janabi kuhusu uhaba wa sukari yazua jambo

**Na Christina Mwakangale**

SUKARI ni kiungo kinachotumiwa katika mlo wa kila siku, hasa kwenye vimiminika tofauti. Kwa walio wengi hutegemea sukari kutengeneza kifungua kinywa, chai.

Kwa watoto wadogo sukari ndio kiungo muhimu zaidi kwao kwa kuwa huwekwa kwenye chakula chao, uji.

Bidhaa ikiendelea kuadimika nchini, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema uhaba wa sukari kwenye maeneo tofauti nchini, ni fursa kiafya.

Kwa siku mbili mfululizo kumekuwa na mjadala mkali mtandaoni baada ya Prof. Janabi kupitia ukurasa rasmi wa MNH Instagram kutoa kauli hiyo iliyoambana na picha yake, akitamka:

“Uhaba wa sukari ni fursa ya kubadili mtindo wa maisha, ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.”

Mjadala umevutia wengi kutokana na jina la aliyetoa kauli hiyo, Prof. Janabi, ambaye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari amekuwa na mvuto kwao, akihimiza jamii kutunza afya kwa kula mlo wenye lishe bora.

“Tunasafisha (dialysis) wagonjwa 120 hadi 130 kila siku ya Mungu Muhimbili. Wagonjwa wanaanza kufika hapa saa tisa usiku. Kisukari, shinikizo la damu,” anataja magonjwa hayo.

Baadhi ya Watanzania walioufuata ukurasa huo na ambao si wafuasi, walitoa maoni yao kadhaa, huku Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, akiupenda ujumbe huo.

‘Usiga’ katika ukurasa wake anasema: “Hii sasa ‘kiki’ daktari, na mwingine akijibu “Ukiwa na akili ndogo hujawahi mwelewa jamaa.”

‘Dk. Fransine’ alisema: “Katika afya ni sawa, lakini katika siasa haimaanishi vizuri,” huku ‘Alexmoshi59’ akisema: “Ninaomba kwenye sukari pawekwe onyo kama kwenye paketi ya sigara. Pia wasiotumia sukari wapunguziwe gharama za bima.”

Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameunga mkono hoja hiyo ya Prof. Janabi, kuhusu jamii kuepukana na matumizi ya sukari, hasa kipindi hiki cha kuadimika kwa bidhaa hiyo.

“Profesa Janabi oyeeee... kwa lugha nyepesi ukimsikiliza Prof. Janabi anasema, mganga mkubwa sana wa masuala ya afya ya binadamu, ulaji wa sukari uliopindukia una madhara kwa afya. Kwa hiyo, wakati huu sukari imeadimika kidogo, achana nayo,” alisema Chalamila.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
20.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya Ijumaa tarehe **23-02-2024 hadi tarehe 29-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia **Mikumi**, gari hizo zina namba za usajili:

**T 112 EAG / T 879 EAU**
**T 778 EAP / T 568 EAZ**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 4.50**
**Kimo - mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
19.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 24.02.2024 hadi 01.03.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea Bandari ya **Dar Es Salaam**, gari hilo lenye namba za usajili.

**NRB97300 / NRB15200**
**DS00TG-GP/ NRB43293**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 36.5**
**Upana - mita 4.3**
**Kimo - mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: **Mzenga** hadi Bandari ya **Dar Es Salaam** kupitia Barabara ya **Morogoro**, Barabara ya **Mandela** gari litasafiri muda wa mchana **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
20.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe **17-02-2024 hadi 18-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga** kupitia **Mlandizi** gari hiyo ina namba za usajili:

**T 792 DYL / T 394 DVS**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 4.50**
**Kimo - mita 4.60**

2. Njia zitakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga kupitia Mlandizi gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**HABARI KITAIFA**

# Mjane wa 'nyama ya swala' kupatiwa mtaji wa biashara

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ZIKIWA zimepita siku nne tangu Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa kumwachia huru mjane Maria Ngoda, mkazi wa Isakalilo, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, mama huyo ameanza kupatiwa msaada.

Mjane huyo alihukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa kifungo cha miaka 22 gerezani kwa kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala.

Jana Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Isiyo ya Kiserikali ya Sauti ya Haki Tanzania, Wakili Leatitia Petro pamoja na Mwakilishi wa Kampuni ya Uwakili ya BLS Attorneys and Partners, Glory Mwandelema, walifika nyumbani kwa mjane huyo ili kumpatia mtaji wa biashara.

Wakili Leatitia alisema pamoja na kuwa alikuwa ni mmoja wa mawakili wa Chama cha Wanasheia (TLS) waliohusika kumtetea mjane huyo, kupitia taasisi yake ameona ni vyema kumsaidia mtaji ili awe na shughuli maalum ya kufanya itakayomwingizia kipato.

Alisema wako kwenye mazungumzo na kufanya tathmini ya kina ya biashara ambayo ataifanya kwa uhakika na kumpatia kipato.

"Tumefika hapa nyumbani kwake ila mwenyewe hatujamkuta ila tumeacha maelekezo yetu kwa familia yake kwa maana ya dada yake mkubwa ili tuwasiliane naye kujua biashara anayotaka kufanya, tutampa mtaji wote," alisema.

Aliongeza kuwa mtaji huo utatolewa Siku ya Wanawake Duniani mwezi Machi na kuwa mbali na Maria Ngoda, kuna wanawake wengine 10 watakaonufaika na misaada mbalimbali siku hiyo.

Aliomba wadau wengine wanaoguswa kumsaidia mtaji mjane huyo na familia yake kujitokeza kwa kuwa mazingira ya makazi yake yanahitaji msaada mkubwa.

Adelia Myumbilwa, dada wa Maria, akishukuru kwa msaada huo, alisema utakuwa tija kwao kiuchumi. Kwa kuzingatia hali yetu kiuchumi, alisema wapaswa kuwamo kwenye mpango wa kitaifa wa kunusuru kaya maskini, lakini hawamo.

Alibainisha kuwa mbali na msaada huo toka Sauti ya Haki Tanzania, tayari Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa, Fatma Rembo ameshafika na kutoa msaada wa Sh. milioni moja kwa ajili ya kumwezesha mtaji mjane Maria.

Mjane huyo aliachiwa huru na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Elvin Mugeta Ijumaa iliyopita baada ya rufani iliyokatwa na TLS Iringa kushinda.

## Wanafunzi wa kike wakumbukwa ujenzi wa vyumba maalum shuleni

**Na Romana Mallya**

SHULE za Sekondari za Nanyamba na Chawi zilizoko Halmashauri ya Mji Nanyamba mkoani Mtwara zimekabidhiwa vyoo vyenye matundu 12, kikiwamo chumba maalum cha kujisitiri wasichana wakati wa hedhi.

Vilevile, shule hizo zimekabidhiwa taulo za kike 2,500 ili kusaidia wanafunzi wa kike shuleni huko wawapo katika hedhi.

Msaada huo umetolewa na Smile for Community pamoja na Legal Services Facility (LSF) ambao ni waandaaji na waratibu wa mbio za maarufu 'Run for Binti' zilizofanyika mwezi Julai mwaka jana ambazo huratibiwa kila mwaka.

Mkurugenzi wa Smile for Community, Flora Njelekela, akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, alisema mbio hizo zilifanyika kwa lengo la kuweka nguvu na rasilimali za pamoja katika kuwawezesha watoto wa kike kupata hedhi salama.

Pia alisema mbio zililenga kurekebisha miundombinu ya shule ikiwamo kuwapo vyoo salama pamoja na maji ili kulinda na kuboresha hali ya wanafunzi shuleni.

"Makabidhiano hayo yanatokana na kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa vyoo hivyo ambavyo vimeboreshwa zaidi na kuwekewa mabomba na masinki ya kunawia mikono pamoja na chumba maalum cha kubadilishia taulo za kike kwa watoto wa kike," alisema.

Flora alisema walianzisha mbio hizo kwa lengo la kumlinda mtoto wa kike na kumpatia hedhi salama na kumwezesha kuwa na mazingira bora ya kupata elimu na kuongeza ufaulu wake darasani.

"Tunafahamu kwamba vyoo bora ni muhimu sana kwa ustawi na afya ya wanafunzi. Kupitia ujenzi wa vyoo hivi na ugawaji wa taulo za kike kwa kila binti, tunahakikisha wanafunzi wetu wanapata mazingira salama na ya kujifunzia bila kuathiriwa na magonjwa au changamoto za kukosa taulo za kike.

"Tunajisikia furaha kupitia mbio za mwaka jana, tumeziwezesha shule hizi mbili. Niwaombe walimu na wanafunzi kuhakikisha vyoo hivi vinatunzwa vizuri ili vitumika muda mrefu," alisema.

Meneja Rasilimali na Mawasiliano wa LSF, Jane Matinde, alisema kwa zaidi ya miaka 12 wamejikita katika upatikanaji wa haki ikiwamo haki ya elimu na afya bora.

Alisema ndio maana wakaona kuna haja ya kushirikiana na Smile Community katika kuandaa na kuratibu mbio hizo kila mwaka na kuomba wadau wengine kuunga mkono.

Ofisa Tarafa wa Nanyamba, Sefu Nayembe, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, alishukuru LSF na Smile Community kwa kukamilisha ujenzi wa vyoo na kugawa taulo za kike kwa shule hizo.

"Pia ninawashukuru kwa kuweka chumba (maalum) cha kubadilishia taulo za kike kwa wasichana, hii itawezesha wanafunzi kujifunza vizuri na kutopata shida yoyote wawapo kwenye hedhi na kusababisha kufanya mitihani yao vizuri," alisema.

Nayembe alisema alitoa wito kwa jamii kuunga mkono jitihada za serikali kama walivyofanya wadau hao katika sekta ya elimu.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nanyamba, Faima Abdallah, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema, "ninawashukuru sana LSF na Smile for Community kwa kutujengea vyoo na kugawa taulo za kike kwa ajili ya kutusaidia tukiwa kwenye hedhi.

"Hii itatusaidia sana tukiwa masomoni kufanikisha ndoto zetu pasipo kupata changamoto yoyote ile," alisema.

Waraka wa Elimu Na. 4 wa Mwaka 2022 unatilia mkazo uimarishaji mazingira ya shule kuwa salama na wezeshi katika ufundishaji na ujifunzaji.


**ARM AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD**

**MARUDIO YA TANGAZO LA TAREHE 9/12/2023**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MuCoBa Bank Plc** TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA TAREHE 20-02-2024 NA KUENDELEA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA.

| NO | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | TAWI ALILOKOPA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA/ MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | JOEL KIBELENGE LUGANGILA | JOEL KIBELENGE LUGANGILA | MAFINGA | SHAMBA NA MABWAWA YA KUFUGIA SAMAKI NA NYUMBA | MAFINGA SAO HILL | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 2 | ALEXANDER JOHN SEYARI | ALEXANDER JOHN SEYARI | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA - BOMA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 3 | ABDALAH MSAFIRI NZINGO | MSAFIRI NZINGO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - CHANGARAWE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 4 | AMOS SANGA | AMOS SANGA | ILULA | NYUMBA | IRINGA - ILULA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 5 | METHEW NALOLE | METHEW NALOLE | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA - CHANGARAWE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 6 | JOEL PETER MAKOLO | JOEL PETER MAKOLO | MADIBILA | NYUMBA | MADIBILA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 7 | LUSANI LUTEGO | VASCO KIVEMBELE | MAFINGA | NYUMBA NA SHAMBA | NYOLOLO - IHANGANATWA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 8 | REUBEN MWAKASALA | REUBEN MWAKASALA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – IHONGOLE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 9 | BONIFACE CHUMO | BONIFACE CHUMO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - GANGILONGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 10 | GAI GAMBA | GAI GAMBA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - CHANGARAWE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 11 | CHARLES MASHITA | CHARLES MASHITA | MAFINGA | NYUMBA | MAFNGA - IHONGOLE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 12 | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | GASTON RUGUGA NTAMAKILILO | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - RUNGEMA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 13 | DICKSON MASASI | DICKSON MASASI | MAFINGA | KIWANJA | MAFINGA-CHANGARAWE<br>MAKALALA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 14 | STEWART MAGILI | STEWART MAGILI | MAFINGA | NYUMBA | MUFINDI SAWALA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 15 | MARRY NGELULA | MARRY NGELULA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 16 | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | MAFINGA | NYUMBA MBILI | MAFINGA – BOMA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 17 | VAILETH GEORGE HAULE | GREGORY MWINDI | MAFINGA | PAGALE | MAFINGA RUNGEMABA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 18 | FABIAN GOFREY YERINDE | JOEL LUGANGILA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – IHONGOLE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 19 | FILBERT YOVENARY KALINGA | FILBERT YOVENARY KALINGA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA - UPENDO | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 20 | MUSA MAKWETA | MUSA MAKWETA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – CHANGARAWE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 21 | HAJI NYAKWILOLA | HAJI NYAKWILOLA | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – BOMA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 22 | ISAYA CUPPUSWAMY | ISAYA CUPPUSWAMY | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – WAMBI LUGANGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 23 | YUSUPH MKULU | YUSUPH MKULU | MAFINGA | NYUMBA | SADANI – UYELA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 24 | MUFINDI INSTITUTE OF AGRICULTURE | MUFINDI INSTITUTE OF AGRICULTURE | MAFINGA | SHAMBA LENYE MAPAGALE YA CHUO EKARI 12 | MAFINGA – BOMA NDOLEZI | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 25 | MENERICK BEATUS BALAMA | MENERICK BEATUS BALAMA | IRINGA | NYUMBA | IRINGA – KILOLO | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 26 | JOCTAN NYALUKE | JOCTAN NYALUKE | MAFINGA | NYUMBA | MAFINGA – BOMA KIGAMBONI | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 27 | AZIM HALID MBONAGA | AZIM HALID MBONAGA | MADIBILA | PAGALE | MADIBILA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 28 | GAUDENCE CHARLES MOHELE | GAUDENCE CHARLES MOHELE | MADIBILA | NYUMBA | MADIBILA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA (25%) AU ZAIDI BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI (75%) ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA.

**MAWASILIANO: 0757 -107 715, 0784 -759 892**




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Akili Platform, Roghat Robert na Balozi wa shirika, Pili Edward (wa pili kushoto), wakikabidhi msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo mfuko wa sabuni ya unga kwa watumishi wa Hospitali ya Mkoa wa Tabora hivi karubini. Kushoto ni Mtaalamu wa Afya ya Akili, Edina Aswile na Hawa Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tafakuri ya Bagonza maziko ya Lowassa

## •Aorodhesha mambo 10 aliyoona Monduli

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Dayosisi ya Karagwe ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Benson Bagonza ameorodhesha mambo 10 yaliyojiri wakati wa maziko ya mwili wa Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa ambaye kifo chake kilitangazwa Jumamosi ya wiki juzi.

Katika andiko lake alilolipa kichwa cha habari kinachosomeka 'EDWARD KAMA EDWARD', Askofu Bagonza anasema:

Jana 17/2/2024 tumemzika Edward Lowassa nyumbani kwao Monduli. Miaka 40 iliyopita tulimzika Edward Sokoine katika eneo hilo hilo la Monduli. Tulivyomzika Edward yule, ndivyo tumemzika Edward huyu. Jina "Edward" lina maana kubwa katika eneo hilo hata kama siijui.

Yalikuwa ni mazishi yenye hadhi. Usingejua kama ni ya Waziri Mkuu mstaafu. Waziri Mkuu yeyote aliye madarakani bado yangemfaa. Yaliandaliwa chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu aliye madarakani - Majaliwa Kassim Majaliwa. Kazi nzuri.

Miongoni wa waliohudhuria mazishi ni huzuni, fahari, furaha, aibu na fundisho. Nilitafakari haya;

**Kwanza;** Edward aliondoka Monduli mara ya mwisho akiwa amesimama. Amerudi amelala. Kulala na kusimama; yote mawili yana nguvu na hadhi sawa. Tuwe wanyenyekevu.

**Pili;** Edward ameliunganisha taifa letu japo kwa siku moja. Wote tulikaa kwa adabu na utulivu na kusahau kwa muda tofauti zetu. Wote tulitumia "washroom" (msalani) zilezile bila kubaguana. Kumbe inawezekana?

**Tatu;** tangu afariki dunia hata mitandao inasema uzuri wa Edward. Imejikita kuwazodoa wanaodhaniwa ni wabaya wa Edward. Fupisheni hukumu zenu juu yao. Yawezekana aliisha wasamehe.

**Nne;** Mishangao yangu: Kutowaona niliodhani wangekuwapo. Kuwaona niliodhani hawawezi kuwapo. Kupopoa historia ya Edward iliyobeba haiba yake ya UAMUZI MGUMU.

**Tano;** mazishi ya Edward Sokoine yalihudhuriwa na Oliva Tambo (Rais wa ANC ya wakati huo) na Alfred Nzo (Katibu Mkuu wa ANC wakati huo). Wageni wa nje waliohudhuria mazishi ya Edward Lowassa ni magavana wa Kimasai kutoka Kenya.

**Sita;** ilipigwa mizinga: Mimi nilihesabu 16, jirani yangu akahesabu 17. Jirani wa upande wa pili akasema ilitakiwa 21. Timu ya wana itifaki wa serikali na jeshi wakawatahadharisha wenye mimba (ujauzito); wakasahau tuko wajinga wengi tusiojua mizinga 16/17 au 21 ina maana gani? Akifa mwingine mtueleze tafadhali!

**Saba;** Freeman Mbowe "aliiba onesho" msibani. Alipata fursa kusalimia kama mwanafamilia. Akainadi Chadema. Akaboresha historia ya Edward. Mama akaikamilisha. Siku yenye huzuni ikaisha vizuri. Tukasikia makofi msibani.

**Nane;** tulipomzika Edward Sokoine, tulizika darasa la uongozi. Kwa kumzika Edward Lowassa, twaweza kuwa tumezika maabara ya uongozi. Mmoja aliamini katika ufukara mtakatifu. Mwingine katika utajiri-uzalendo. Tusihemuke, tutafakari.

**Tisa;** Edward huyu ameacha msiba kuliko msiba wa kifo chake. Tuna kizazi cha viongozi vijana na wazee vijana. Hawa Mungu wao ni tumbo na mbingu yao ni madaraka. Upo uhusiano wa matumbo yao na dhamana waliyopewa: Matumbo yao yanapanuka wakati dhamana na taasisi zao zinakonda. Hawana kiu ya haki tena.

**Kumi;** Monduli ilikuwa ndogo siku ya mazishi. Msiba ukahamia kwenye ng'ombe. Watu walizoea kula nyama alipokuwa hai. Wamekula zaidi alipokufa. Tupo ambao hatukusikia njaa pamoja na kutokula. Kwaresima ya 2024 tutaikumbuka kwa kushinda njaa tukikuzika. Fredy Lowassa umuenzi babako daima kwa kuwapa watu nyama walizozizoea alipokuwa hai.

Katika kuhitimisha andiko lake, Askofu Dk. Bagonza anasema: "Nilitamani mmoja toka familia ya Edward Sokoine aongee na kutufariji.

"Nilitamani aliyemteua kuwa Waziri Mkuu atusalimie. Haikutokea. Ukisikia msiba, hiyo ndiyo maana yake. Ukipenda, mnyime mengine lakini ni muungwana sana. Alihudhuria. Tumalize matanga, maisha yaendelee."

## Waiba nguo za wanaojifungulia Kituo cha Afya

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

KITUO cha Afya Mafiga ambacho kinatoa huduma kwa wananchi wa kata zaidi ya saba za Manispaa ya Morogoro, kinakabiliwa na changamoto ya kukosekana chumba ya upasuaji na uzio, hali inayosababisha baadhi ya watu kukatisha ndani ya kituo na wengine kuiba nguo zinazoanikwa na kinamama walioijifungua.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Naojwa Kimaya, alibainisha hayo wakati akitoa maelezo ya utendaji kazi kwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, Nora Mzeru aliyekabidhi mashuka kwa ajili ya wagonjwa.

Mbunge huyo aliambatana na Diwani wa Mafiga, Thomas Butabile na viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) ngazi ya kata na wilaya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Dk. Kimaya alisema watu kukatisha ndani ya eneo la kituo hicho si salama kwao kwa sababu wanaweza kupata magonjwa mengine ya watu waliyonayo.

Alisema kutokana na kukosekana uzio huo, baadhi ya watoto kutoka kwenye makazi yanayozunguka kituo hicho wamekuwa wakiingia ndani ya kituo na kucheza, hali ambayo ni hatari kwa afya zao.

Dk. Kimaya alisema kuwa wakati mwingine watu wanapita ndani ya kituo, baadhi yao wanaiba nguo za wagonjwa zilizoanikwa.

"Tuna changamoto kubwa sana, wapo kinamama wanaokuja kujifungua, wanafua nguo zao na wanazianika kwenye kamba, wanapozungukia jengo wanakuta hazipo, wezi wameiba. Hivyo, tunatamani kuwa na uzio ambao ni imara ili kuzuia hizo changamoto zote," alisema.

Dk. Kimaya alisema kuwa kituo kilianza kikiwa na hadhi ya zahanati na baadaye kufikia ngazi ya kituo cha afya na kwa sasa kinapokea wagonjwa wengi wa nje wanaofikia 2,000 hadi 3,000 kwa mwezi. Hakilazi wagonjwa wa nje isipokuwa wanawake wanaofika kujifungua.

Alibainisha kuwa kituo kina vitanda 24 kwa ajili ya wanawake wanaojifungua ambao kwa mwezi ni kati ya 250 na 300.

"Kutokana na wingi wa wagonjwa na sisi tunatamani tuwe na chumba cha upasuaji ili kupunguza usumbufu ambao wateja wetu wanapata wa kuwatoa hapa kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa," alisema Dk. Kimaya.

Mmoja wa kinamama wajawazito wanaopata huduma katika kituo hicho, Mwajuma Habibu, alisema kutokana na changamoto hiyo ya wezi, wanalazimika wanapofua nguo, wanasubiria mpaka zikauke na kuzianua. Akaomba serikali kujenga uzio katika kituo hicho cha afya.

## CRDB, waandishi wa habari kuchochea ujumuishi kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuendeleza sekta ya habari nchini, Benki ya CRDB imeendesha semina maalum kwa wadau wa sekta ya habari nchini na uchumi 'CRDB Bank Media Day' iliyofanyika katika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam.

Akifungua semina hiyo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema CRDB Bank Media Day ya mwaka huu imejikita katika kuangazia ripoti ya Finscope 2023 na namna vyombo vya habari vinaweza kuchochea ujumuishi nchini.

"Ripoti ya Finscope ya 2023 inaonesha ujumuishi wa kibenki upande wa huduma za benki ni asilimia 22 tu pamoja na jitihada na ubunifu mkubwa katika bidhaa.

"Hii inaonesha kuna ombwe kubwa la elimu ya fedha, hivyo leo (jana) tumepata kujadili ni namna gani wenzetu wa sekta ya habari wataweza kusaidia kutoa taarifa na huduma za fedha," alisema Nsekela.

Katika semina hiyo, waandishi wa habari walipata fursa ya kupata mafunzo ya namna ya bora ya kuandaa na kutoa mafunzo ya taarifa za biashara, fedha na uchumi. Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za benki hiyo katika kusaidia kujenga waandishi mahiri nchini.

Akizungumza katika semina hiyo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alipongeza Benki ya CRDB kwa kuandaa semina hiyo iliyowaleta wadau wa sekta ya habari kujadili namna ya kuongeza mchango wake katika maendeleo hususani katika kuongeza ujumuishi wa kifedha nchini. Matinyi aliwahakikishia wadau wa sekta hiyo kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri yatakayosaidia kuboresha sekta ya habari.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa katika semina hiyo ikiwamo 'Jukumu la Vyombo vya Habari katika Kuchochea Ujumuishi wa Kifedha' iliyowasilishwa na Mhariri mstaafu wa Nationa Media Group Kenya, Charles Onyango Obbo, 'Elimu ya Fedha kupitia Mitandao ya Jamii' iliyowasilishwa na Fayness Sichwale, mshauri wa masuala binafsi ya fedha na Mwanzilishi wa Personal Finance Hub na 'Usomaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha' iliyowasilishwa na Dk. Ndalahwa Masanja, Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha ESAMI.

Katika semina hiyo iliyohudhuriwa na waandishi na wahariri kutoka vyombo mbalimbali nchini, Benki ya CRDB pia imezindua shindano maalum la kutafuta waandishi wa habari wachanga wa habari za biashara, fedha na uchumi. Shindano hilo ambalo litaendeshwa kwa muda wa miezi miwili hadi Aprili 12, 2024, litatoa washindi watatu ambao watajishindia zawadi ya Sh. milioni moja na nafasi ya kufanya kazi na Benki ya CRDB.

Vilevile, katika hafla hiyo, Benki ya CRDB imetoa tuzo za kutambua mchango wa waandishi wa habari wawili nguli katika sekta ya habari nchini. Waliokabidhiwa tuzo hizo ni Eda Sanga, mwandishi mstaafu wa Shirika la Habari la Tanzania (TBC) na Mwenyekiti wa Umoja wa Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), na Ndimara Tegambwage, mwandishi wa zamani wa magazeti ya Uhuru na Mzalendo na mmoja wa waanzilishi wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA).

SHERIA MPYA

# Rukhsa mafao kuwa dhamana mkopo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA



MUSWADA wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii (2024), umesomwa kwa mara ya kwanza bungeni, ukiwa na mapendekezo yanayojumuisha sehemu ya mafao kutumika kama dhamana ya kisheria.

Katika pendekezo hilo, inafafanuliwa kutolewa rukhsa kwa mwanachama ambaye hajafikia umri wa kustaafu, kutumia sehemu ya mafao yake kama dhamana ya mkopo wa nyumba.

Lengo la marekebisho hayo ni kutoa ufafanuzi kwa kuwa vifungu vya 52 na 76 vinazuia matumizi ya mafao kama dhamana ya mkopo isipokuwa kwa mkopo wa nyumba kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 20.

Muswada huo uliwasilishwa bungeni mwishoni mwa wiki na serikali na kusomwa kwa mara ya kwanza.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alielekeza muswada huo kushughulikiwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Muswada huo pia unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kuweka masharti bora ya usimamizi wa mifuko.

Inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 11A ili kuwezesha watu waliojiajiri wenyewe katika sekta binafsi kujiunga na kunufaika na mafao ya hifadhi ya jamii katika mpango wa uchangiaji kwa mujibu wa sheria ili kuongeza wigo wa Hifadhi ya Jamii kwa watu waliojiajiri.

Inapendekezwa katika muswada huo kurekebisha kifungu cha 12(1) ili kuainisha asilimia za kiwango cha uchangiaji kinachopaswa kuwasilishwa na mwajiri kwenye mfuko.

Muswada unapendekeza kufuta kifungu cha 12(3) ili kuruhusu mwajiri kuchangia kwa kiasi kikubwa au kiasi chote. Kifungu cha 12(5) kinapendekezwa kurekebishwa kuainisha namna ya uchangiaji kwa wanachama waliojiajiri.

Vilevile, inapendekezwa katika muswada huo kuongeza kifungu cha 12A ili kutoa rukhsa mfanyakazi aliyeajiriwa na mwajiri zaidi ya mmoja kuchangiwa na waajiri wote kwa ridhaa yake ili kumpa mwanachama uhuru wa kuchangiwa na zaidi ya mwajiri mmoja.

"Kifungu cha 14(3) kirekebishwe ili kupunguza adhabu ya tozo kutoka asilimia tano hadi asilimia mbili na nusu inayotozwa na mfuko kwa mwajiri kwa kuchelewa kuwasilisha michango ya mfanyakazi ili kuainisha kiasi stahiki cha faini. "Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka wajibu kwa Mkurugenzi Mkuu wa kuhesabu kuwa kiwango chote kimewekwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hata kama kiwango hicho kilikatwa na mwajiri na hakikuwasilishwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili kulinda maslahi ya wanufaika wa mafao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii," inapendekezwa katika muswada huo.

Pamoja na hayo, inapendekezwa pia kufuta na kuandika upya kifungu cha 16 kufutwa na kuandikwa upya ili kubainisha kwa ufasaha masharti yanayohusiana na malipo yaliyofanyika kimakosa ili kuboresha usimamizi wa michango iliyopokewa kimakosa kwenye mfuko huku kifungu cha 20(3) kikipendekezwa kufutwa kwa kuwa maudhui yake yanakinzana na taratibu za mfumo wa pensheni.

Kifungu cha 23 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuruhusu michango iliyowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi kufikia miaka 70 kuzingatiwa katika ukokotoaji malipo ya mafao ya pensheni ili kuongeza wigo wa upatikanaji mafao ya pensheni kwa mwanachama ambaye amefikisha umri wa kustaafu, lakini hajakidhi vigezo vya kupata pensheni na amekuwa akichangia kuanzia umri wa miaka 61 mpaka 70.

Kifungu cha 28 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha mafao ya ulemavu kwa wanachama ambao wana ulemavu wa kudumu kutokana na majeraha au ugonjwa usiotokana na kazi.

Kifungu cha 28A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha Mkurugenzi Mkuu kuteua jopo la madaktari ili kuthibitisha iwapo mwanachama amepata ulemavu wa kudumu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa mafao yanatolewa kwa mnufaika anayestahili.

Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta maneno 'thirty three' na kuweka maneno 'thirty six' ili kuongeza kiwango kinacholipwa kwa wategemezi pale ambapo mwanachama atakuwa amefariki.

Kifungu cha 72 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza makosa mapya kwa mwajiri anayekataa kujiandikisha na mtu yeyote anayemzuia mkaguzi wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hicho pia kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka au ofisa wa mfuko aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua kesi yoyote ya jinai chini ya sheria ili kuhakikisha utekelezaji na usimamizi bora wa sheria.

Kifungu cha 74A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka mdaiwa kuweka dhamana ya gharama anapoomba rukhsa ya kujitetea katika kesi za kurejesha michango ili kuhakikisha upatikanaji michango ya wanachama, shauri dhidi ya mwajiri linapomalizika.

Katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, katika kifungu cha 5(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti; waajiriwa wa kampuni ambayo serikali inamiliki angalau asilimia 30 ya hisa ni lazima wasajiliwe kwenye mfuko.

Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiwezesha bodi kuondoa michango ya ziada iliyoainishwa chini ya sheria ili kutoa nafuu kwa taasisi zilizoonesha nia ya kutekeleza masharti ya sheria, lakini zinashindwa kulipa adhabu za faini kutokana na changamoto za kifedha.

Kifungu cha 45 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kwamba mnufaika wa mafao ambaye kwa kipindi husika anatumikia kifungo, anaweza kuridhia kwa maandishi kwamba mafao yake au sehemu yoyote ya mafao ilipwe kwa mnufaika atakayetajwa.

Kifungu cha 47 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti yanayohusiana na kutokuhamishika kwa mafao ya wanachama ili kutoa ufafanuzi, kulinda ustawi wa wanachama na mafao yao.

Kifungu cha 48 kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa dhana ya mafao yasiyodaiwa haitumiki kwenye kanuni za msingi za hifadhi ya jamii ili kumwezesha mnufaika kudai mafao yake pasipo na ukomo wa muda.


Kifungu cha 58 cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuboresha masharti yanayohusiana na utekelezaji mapendekezo ya uthaminishaji wa ustahimilivu wa mfuko.

Katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, katika kifungu cha 42(3) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuruhusu vyama vya wafanyakazi au mtu mwingine yeyote kuwawakilisha waajiriwa katika madai ya fidia katika mfuko ili kuzuia mgongano wa maslahi kwa kuwa maofisa ajira na moafisa wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi ni sehemu ya watu wanaotekeleza sheria hiyo.

Kifungu cha 48(6) kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha mwajiriwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu kuendelea kupokea pensheni hata baada ya kurejea kazini au kupokea mafao ya uzeeni ili kuweka usawa kati ya wanufaika ambao wanapokea mafao kwa mkupuo na wanaopokea pensheni.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Hoja hii ya Mbunge Mpina ina mashiko, ifanyiwe kazi

**MJADALA** mkali uliibuka bungeni wiki iliyopita kuhusu upasuaji kurekebisha maumbile, ikiwamo kupunguza au kuongeza ukubwa wa makalio katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa (CCM), ndiye aliyeibua zogo bungeni, alipotoa hoja kwamba MNH-Mloganzila imeanzisha huduma hiyo kinyume cha Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007.

Hospitali hiyo ilitangaza kuanza upasuaji huo wa mapambo 'Reconstructive Cosmetic Surgery' Oktoba 27, mwaka jana.

Mbunge Mpina, aliyewahi kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika awamu ya kwanza ya uongozi wa Rais John Magufuli, alihoji sababu za uongozi wa hospitali hiyo kutoa rukhsa ya jambo hilo wakati hakuna mahali kwenye Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 imetoa baraka vituo vya afya nchini kuwa na huduma hiyo.

Ni hoja iliyoibua si tu hisia za wabunge wenzake waliosimama bungeni na kuchangia mjadala, bali pia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Naibu wake, Dk. Mollel, waliolazimika kutoa ufafanuzi, ambao hata hivyo, haukujibu hoja kuu - huduma inatolewa kinyume cha Sera ya Taifa ya Afya.

Mbunge Mpina alikwenda mbali zaidi, akisema serikali imeanzisha huduma hiyo bila kibali cha Bunge na hakuna sheria, kanuni na mwongozo wa utoaji huduma hiyo.

Nipashe, tukiwa wadau katika sekta ya afya, tunaona hoja ya Mbunge Mpina ina mashiko na inapaswa kufanyiwa kazi na serikali.

Tunatambua kwamba kila aina ya matibabu inayotolewa kwenye vituo vya afya nchini, imewekewa mwongozo mahususi kuanzia aina ya vipimo hadi dawa wanazopaswa kupatiwa wagonjwa; ziwe za sindano, vidonge au kunusa.

Ukirejewa ufafanuzi uliotolewa na mawaziri wenye dhamana ya afya dhidi ya hoja ya Mbunge Mpina bungeni wiki iliyopita, ni wazi kwamba huduma hiyo mpya MNH-Mloganzila haina mwongozo wa kitabibu nchini.

Hatari iliyopo ni kwamba watu watakaopatiwa matibabu hayo, wakipata madhara, hakuna sheria inayowaongoza matabibu katika kutoa huduma hiyo. Ndipo penye hoja ya Mbunge Mpina.

Tunapongeza uamuzi wa serikali kutoa huduma hiyo ya kitabibu nchini ili kuwapunguzia gharama wananchi waliokuwa wanalazimika kwenda ughaibu kusaka huduma hiyo, lakini kama tulivyodokeza awali, matibabu yoyote lazima yawe na mwongozo wa kisera.

Ni katika muktadha huo, tunaona hoja ya Mpina ina mashiko. Inapaswa kufanyiwa kazi na serikali ili kuhakikisha huduma hiyo mpya kitabibu nchini inatolewa pasi na kukwaza sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya nchi katika eneo la tiba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuwaandae watu wetu kustaarabika

Na Restuta James

**JIJI** la Dar es Salaam ambalo ndilo kitovu cha biashara cha taifa na nchi jirani zisizo na bandari, naweza kusema linaongoza kwa kutokuwa na ustaarabu na hata usafi wa mazingira.

Ukiingia Ubungo kilomita chache kabla ya kuifikia Kariakoo kwenye soko la kuzihudumia Zambia, Malawi, DRC na Uganda ambazo ni miongoni mwa nchi zisizo na bandari utashangazwa na jinsi majengo ya mabati yenye kutu na machakavu, kuta zilizobomoka, vibanda vibovu vya biashara vinavyokulaki na kukualika kuingia Dar.

Baada ya hayo inafuata kero ya 'maandamano ' yasiyokwisha. Kila mahali ni msongamano mkubwa wa watu iwe masokoni na katika vituo vikubwa vya daladala na barabarani kunaongoza kwa kuanika 'upungufu uliozidi' kwenye mikakati hafifu ya kuitoa nchi kwenye ushamba kwenda kwenye werevu wa mipango miji na kimaarifa.

Ninaandika haya nikiamini kwamba serikali ikiamua 'kutustaarabisha' inawezekana kwani kinyume chake tunalea udhaifu na kuitukanisha nchi na jiji letu kwa wageni ambao wangepaswa kujifunza kwetu.

> **Ninaandika haya nikiamini kwamba serikali ikiamua 'kutustaarabisha' inawezekana kwani kinyume chake tunalea udhaifu na kuitukanisha nchi na jiji letu kwa wageni ambao wangepaswa kujifunza kwetu.**

Kwa mfano, ukifika Mbagala Rangitatu utakutana na wamama wamepanga ngogwe, nyanya, vitunguu na kila bidhaa ya jikoni, kwenye njia ya watembea kwa miguu na hapo hapo kuna 'dampo' mtu mwingine anamwaga majivu na kiporo cha maharage yaliyochacha.

Pembeni yake kuna mwingine anauza nguo za watoto, amepakana na anayeuza foni za masikioni na makava ya simu ambaye naye ana jirani anayeuza juisi ya miwa. Wakati unajiuliza ukwepe majivu au harufu mbaya ya 'dampo' kuna daladala linakupigia honi maana upo barabarani. Wakati huo huo, kuna mpigadebe anakuhimiza upande kwenye gari kwani ni ya 'moja kwa moja.'

Hali ni hiyo hiyo katika soko la Kariakoo karibu yote ambayo ndiyo nitakayoizungumzia zaidi katika maoni yangu.

Kariakoo ambayo ni soko la kimataifa, imegeuka gulio la kuuza ndizi za kuchoma, viazi, mihogo, ugali na mishikaki kwenye matoroli barabarani hadi kila aina ya bidhaa. Hoja yangu sio wamachinga, hoja yangu ni mpangilio ya umachinga wenyewe.

Kariakoo huwezi kuingia na kutoka na gari kwa urahisi, hili si jambo bora na lenye afya kwa mustakabali mzima wa kutoka kwenye moja ya maradhi yaliyotangazwa na baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Maradhi ujinga.

Ni lazima wakazi wake na wageni pia, tukisaidiwa na serikali tujifunze kustaarabika kwa kutaka au kutotaka. Nasema hivi kwa sababu, haiwezekani unatembea barabarani, kulia unapishana na mkokoteni ulio na jiko la mkaa linalochoma mishikaki na ndizi, kulia kuna jiko la gesi linasonga ugali, mbele kuna kuli kabeba furushi na nyuma kuna chinga anakubembeleza ununue sendo. Bughdha hii anaipata Mtanzania na mgeni aliyekuja soko la kimataifa kufungasha mzigo wa milioni 100!

Nani wa kulaumiwa hapa? Ni sisi wote na zaidi wenye madaraka na mamlaka ya kupanga mambo kwa niaba ya wengi. Hawajatupanga wala kutustaarabisha. Dunia na hasa nchi nyingi za Afrika zinapambana kuondoa sekta isiyo rasmi lakini sisi ndio kwanza tunaruhusu majiko ya mishkaki yazurure na moto barabarani.

Tunaruhusu wapigadebe watukane matusi ya nguoni 'mchana wa jua kali' bila kujali umri wala yeyote tena wakiwa wamevalia mavazi machafu.

Huu sio uungwana hata kidogo kwa mfano, mtu anatoka Zambia kuja kufuata mzigo, anapapaswa makalio na wahuni ambao wanatumia mwanya wa msongamano 'uliotengenezwa' na kubatizwa jina la umachinga. Hii ni aibu wala si fahari na kitu cha kujivunia kuendelea kukuza sekta isiyo rasmi.

## Imani potofu zatajwa kikwazo matibabu ya midomo sungura

**Na Gwamaka Alipipi**

LICHA ya matibabu kwa watoto wanaozaliwa na tatizo la mdomo wazi kutolewa bila malipo, imeelezwa kwamba imani potofu ni kikwazo cha mwitikio wa wazazi kuwapeleka watoto hospitalini kupata matibabu.

Kulingana na takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), watoto 200,000 kila mwaka wanazaliwa na matatizo ya mdomo wazi, huku Afrika takwimu zikionesha kuwa katika kila vizazi 1,000, mtoto mmoja anazaliwa akiwa na tatizo hilo.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na madaktari bingwa wa upasuaji na madaktari bingwa wa kinywa na meno wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa dawa za usingizi, madaktari wa upasuaji mdomo sungura na manesi yaliyotolewa na Taasisi la Lifebox.

Daktari Bingwa wa Upasuaji Rekebishi Hospitali ya CCBRT, Edward Wayi, alisema kuwa nchini tatizo la watoto wanaozaliwa na mdomo wazi ni kubwa.

Alisema kila mwaka watoto 2,500 wanazaliwa na tatizo hilo. Kati yao, nusu ndiyo wanaopata matibabu.

"Ni tatizo ambalo kwenye jamii lipo ila watu bado wanawaficha watoto kutokana na imani potofu. Pia kuna changamoto ya huduma bora zinazotolewa, kuna hospitali chache zinazotoa huduma hii. Kwa sasa huduma inatolewa Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Dar es Salaam," alisema Dk. Wayi.

Akizungumzia kuhusu visababishi vya ugonjwa huo, Dk. Wayi alisema husababishwa na mwingiliano wa matatizo ya vinasaba na sababu za kimazingira ikiwamo unywaji pombe uliokithiri, utumiaji tumbaku na lishe duni kwa mjamzito.

Pia anasema kuna sababu ya kimazingira ambazo hutokea mama akiwa mjamzito, mama kutopata hewa ya oksijeni ya kutosha wakati wa ujauzito.

Daktari Bingwa wa Dawa za Usingizi Hospitali ya CCBRT, Peter Saria, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajenga uwezo na kuwapa mbinu za kisasa watoahuduma wa dawa za usingizi ili kuhakikisha watoto wenye tatizo hilo wanakuwa salama wakati wa operesheni.

Alisema wataalamu wa dawa za usingizi ni muhimu kwenye matibabu ya watoto hao, umakini zaidi unahitajika wakati wa kumtibu mtoto kuliko mtu mzima, ndiyo sababu wamepewa mafunzo hayo.

Daktari Bingwa wa Kinywa na Meno pamoja na upasuaji wa watoto wenye mdomo wazi Hospitali ya Mkoa Dodoma, Athanas Masele, alisema kwa mtoto aliyepasuka mdomo kwa ndani hufanyiwa operesheni akifikisha miezi tisa.

Alisema: "Tatizo la mdomo wazi au mdomo sungura ni kubwa nchini. Kwa sasa tunatoa elimu kwa jamii ili ihamasike na kuwaleta watoto wenye tatizo hilo ili wapate matibabu."



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga (kulia), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu changamoto ya umeme na kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka juu ya changamoto hiyo. Kushoto ni Ofisa Programu Mwandamizi wa Uchechemuzi na Maboresho wa Kituo hicho, Raymond Kanegene. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# LHRC: Mgawo wa umeme unaminya haki za binadamu

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimesema mgawo wa umeme unaotikisa nchini kwa sasa unaminya haki za binadamu, kikishauri serikali kuchukua hatua stahiki kutatua changamoto ya upungufu wa umeme.

Kimesema kuwa moja ya hatua hizo ni Shirika la Umeme (TANESCO) kupanga ratiba ya matengenezo ya mitambo ya kuzalisha nishati hiyo kwa kuzingatia sayansi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga ndiye aliyetoa ushauri huo kwa serikali mkoani Dar es Salaam jana, alipotoa tamko la kituo hicho kwa waandishi wa habari kuhusu kukosekana kwa umeme na uhusiano wake na haki za binadamu.

"Tunapendekeza pia TANESCO kutoa taarifa zisizokuwa na mkanganyiko, serikali kuongeza uwekezaji katika vyanzo vya uzalishaji nishati ya umeme isiathirike kirahisi na mabadiliko ya hali ya hewa," alisema Dk. Anna.

Alisema pendekezo hilo linalenga upatikanaji endelevu wa nishati hiyo kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji umeme nchini.

"Vilevile, tunapendekeza serikali kuchukua hatua za haraka za kuwezesha upatikanaji umeme ndani ya muda mfupi. Hili linawezana, kwani tumeshuhudia miaka zaidi ya sita ya hivi karibuni nchi ilikuwa na umeme wa uhakika," alisema.

Alifafanua kuwa kituo hicho kimefuatilia na kufanya tathmini hali ya kukatika kwa umeme na athari yake kwenye haki za binadamu na athari za kiuchumi na kufikia kutoa tamko hilo kuikumbusha serikali.

"Kukatika kwa umeme kunaathiri haki mbalimbali za kikatiba ikiwamo Ibara ya 22 na 23 inayobainisha haki ya kufanya kazi na kujipatia ujira, Ibara 14 haki ya uhai kwa kupata afya bora, na Ibara ya 18 haki ya kupokea na kutoa taarifa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema pamoja na jitihada za serikali za kutatua kero ya ukosefu wa nishati hiyo, ni vyema pia kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta utatuzi wa kudumu wa upungufu wa umeme.

Alisema kukatika kwa umeme kumekuwa kukijirudia mara kwa mara licha ya kuwa na utajiri wa vyanzo mbalimbali vya uzalishaji, ikiwamo gesi asilia inayozalishwa Mtwara na Lindi katika maeneo ya Songongo, Msimbati, Mnazibay na Madima.

"LHRC tumetoa mapendekezo yetu kwa serikali kuwa kuendelea kwa mgawo wa umeme kwa kujirudia, kumesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi, hasa katika shughuli za kila siku za maisha kama vile uzalishaji, biashara, huduma za afya na elimu," alisema.

Alisema kumekuwapo ongezeko la gharama za maisha kutokana na wananchi kutumia nishati mbadala ikiwamo jenereta na umeme wa jua, na kwamba wanaweza kukabiliwa na gharama kubwa za kununua na kuendesha vifaa hivyo, pia kupunguza ufanisi wa kiuchumi kwa wananchi.

"Kwa ujumla, kukosekana kwa umeme kunaweza kusababisha athari kubwa kiuchumi na kijamii kwa jamii na uchumi wa nchi, linahitajika suluhisho la haraka na la kudumu ili kuboresha upatikanaji nishati ya umeme," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete wakishirikiana na madaktari wa Hospitali ya AICC kutoa huduma ya kupima moyo katika kambi ya siku sita ya upimaji wa magonjwa ya moyo inayofanyika Hospitali ya AICC jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# BoT: Kuna watu wameficha dola

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imesema nchi haina uhaba wa dola, bali baadhi ya watu wamezihifadhi wakitarajia bei itapanda, ikisisitiza hakutakuwa na ongezeko hilo kutokana na hatua za ndani na nje zinazochukuliwa katika kuimarisha upatikanaji wake.

Imezitaja hatua hizo zinajumuisha uamuzi wa Marekani kulegeza masharti ya riba kwenye masoko yake ya fedha, kupungua kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia na ya nchini na kuendelea kutoa bei elekezi na kufuatilia kwa karibu sekta ya fedha nchini.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Meneja Msaidizi Utafiti wa BoT, Dk. Lusajo Mwankemwa, alibainisha hayo alipotoa mada kuhusu majukumu ya taasisi hiyo benki hiyo wakati wa semina kwa waandishi wa habari, ambao walitaka kujua hatua zinazochukuliwa kuimarisha upatikanaji dola nchini.

"BoT tunajua na tunaona dola zipo ila ni ngumu kukufuata kutaka tuchukue dola nyumbani kwako, mimi (BoT) nitasema dola moja ni kiasi hiki (bei elekezi).

"Siwezi kuja nyumbani kwako wewe uliyezihifadhi nikikwambie lazima kuuza kwa bei hii, BoT jukumu lake ni kutoa mwongozo wa kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikanaje," alisema.

Kuhusu uendeshaji maduka ya kubadilishia fedha, meneja huyo alisema kuwa kwa sasa serikali inapitia upya kanuni ili kulegeza masharti kuwezesha wengi kuyafungua kwa kuwa yanasaidia kukusanya fedha kutoka kwenye jamii na kuzileta kwenye mfumo rasmi wa kibenki.

"Tunachokiona sasa ni watu kuzuia ili ipande bei, hawataki kuiachia lengo ni kupata faida, dola ni bidhaa. Kuna sehemu huenda tulikosea kama serikali pengine tulipofunga maduka ya kubadilisha fedha na sera nyingine na ukichanganya na changamoto zilizotokea duniani ikazidi.

"Changamoto ya dola si ya Tanzania pekee, wananchi na wadau wanafikiri haipatikani, BoT ikitazama kwenye mifumo yao wanaona dola ipo, shida ni wauzaji kutoendana na bei elekezi, ila wanatoa taarifa kwa umma kuhusiana na hali halisi.

"Wanaoficha wajue kuwa dola haitapanda thamani, wanaoificha wanajisumbua, ndani ya kipindi kifupi itaonekana kuficha dola si faida, sasa ili tuzitoe mifukoni mwao ziingie kwenye mzunguko ndo tunapitia vigezo vya kuanzisha maduka ya kubadilisha fedha ili fedha ziingie huko," alisema Dk. Mwankemwa.

Kwa muda mrefu kumekuwa na kilio cha ugumu wa kupata dola nchini huku BoT ikisisitiza kuwa zipo na akiba iliyopo nchini ni Dola za Marekani bilioni 5.3 inayotosha kwa miezi mitano ijayo.

Februari 7, mwaka huu, Mkurugenzi wa Utafiti na Sera wa BOT, Dk. Suleiman Missango, alisema: "Kuna upungufu wa fedha za kigeni, lakini bado ni himilivu.

"Hali haijatengemaa, hivyo majibu yetu ni kama ya mwaka jana kwamba akiba tuliyonayo inatutosha kulinganisha na majirani zetu. Hakuna sababu ya wananchi kupaniki.

"Safari hii hatujanunua dola sokoni. Kwahiyo, ile iliyoingia kupitia utalii na export (mauzo ya nje) ya mazao tumeiacha kwenye mzunguko," alifafanua.

Alibainisha kuwa Novemba hadi Desemba mwaka jana, nchi ilipata Dola za Marekani kutokana na msimu wa utalii ulioingizia nchi fedha za kigeni pamoja na uuzaji mazao ya biashara nje ya nchi.

Alisema mazao ya korosho, pamba na tumbaku yameingizia nchi fedha za kigeni, ambazo serikali iliamua zibaki kwenye mzunguko badala ya kupelekwa BoT.

"Sisi kama BoT tunaona hali ya fedha za kigeni haijabadilika sana tangu tulivyoongea... hizi changamoto zinatokana na sababu za nje ya nchi zaidi.

"Hatuna haja ya kupaniki, hatuko kwenye hali mbaya. Sisi ni kama mgonjwa ambaye ameshaanza matibabu kutokana na mikakati tuliyonayo pamoja kupokea mikopo na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo," alisema.

Dk. Missango alisema taarifa zilizopo mitaani ndizo zinasababisha taharuki na uhaba wa dola kinyume cha hali halisi, jambo linalofanya bei ya dola ipande.

"Ukituuliza sisi tunaona Marekani na Ulaya, mwanzoni walikuwa wanapandisha riba, hivyo mitaji ilikuwa inaelekea huko, lakini sasa wameanza kusitisha. Kwahiyo, baada ya muda uhaba utaondoka kwa sababu fedha zilizokuwa zinatoka kwenye nchi zetu hazitakuwapo kwa kiasi hicho," alisema.

Mwaka jana, Benki Kuu za nchi zenye uchumi mkubwa duniani zilipunguza ukwasi katika uchumi huku Marekani ambayo ndiyo inachapisha dola ikiongeza riba kutoka asilimia 0.75 hadi asilimia 5.2, ambalo ni ongezeko la asilimia 500.

Alisema katika kipindi cha miezi mitatu ijayo, upatikanaji dola utaimarika zaidi kwa kuwa nchi itaingia kwenye msimu wa utalii.

Dk. Missango alisema taarifa ya maoteo ya mwenendo wa uchumi wa dunia iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha duniani (IMF) pamoja na mashirika mengine ya kimataifa inaonesha kwamba bei za mafuta na bidhaa nyingine zitashuka.

Akizungumzia uuzaji wa dola kwenye benki, Dk. Missango alisema msimu wa utalii na wa mauzo ya nje uliifanya BoT kutokuuza dola kwenye benki kwa kuwa kiasi kilichoingia nchini, kiliingia moja kwa moja kwenye mzunguko sokoni.

Alisema BoT inafuatilia mwenendo wa upatikanaji dola na kwamba hatua nyingine ni kuendelea kununua dhahabu serikalini, kuuza akiba ya Kwacha za Zambia zilizopo kwenye akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania iliyopo Benki Kuu ya Zambia, kupunguza ukwasi wa shilingi kwenye uchumi na kutoa leseni za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni katika maeneo mengi nchini ili kuongeza fedha za kigeni kwenye mzunguko rasmi.

## Waziri akabidhi magari kuboresha miliki ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amekabidhi magari 16 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.079 yatakayosaidia kupunguza gharama za kukodi magari wakati wa utekelezaji Mradi wa Uboreshaji wa Miliki za Ardhi (LTIP).

Mradi huo wa uboreshaji milki za ardhi utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, ukigharimu zaidi ya Sh. bilioni 346 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB).

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi magari hayo iliyofanyika mji wa kiserikali Mtumba jijini hapa, Silaa alisema tangu uhuru, Tanzania haijawahi kupata mradi mkubwa kama huo katika sekta ya ardhi.

Alisema magari hayo 16 yatasaidia kuharakisha utekelezaji mradi huo ambao umejikita katika kuboresha milki za ardhi mijini na vijijini.

"Mradi huu utakwenda kuwa suluhu kubwa katika sekta ya ardhi kwani utasaidia kupima pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini na kutoa hati miliki kwa wananchi," alisema Silaa.

Waziri Silaa alimwagiza mratibu wa mradi huo kuhakikisha kuwa magari hayo yanatumika kwa matumizi yaliyopangwa na si vinginevyo.

"Bahati nzuri hivi sasa nchi yetu kila mtu ni mwanahabari, magari haya kama yatafanya matumizi tofauti, tutaona tu! Hivyo basi niwaombe yaende kufanya kazi zilizokusudiwa ili mradi ukiisha tuyatumie katika wizara yetu kwenye majukumu mengine," alisema Silaa.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anthony Sanga, alisema magari hayo 16 yamenunuliwa ili kurahisisha utekelezaji wa mradi huo. Mahitaji ni magari 75.

"Magari haya 16 ambayo Mheshimiwa Waziri unakabidhi ya mradi huu ni sehemu ya mengine 59 ambayo yataingia bandarini na bei ya kila gari ni Sh. milioni 129.9 na baada ya kukabidhiwa leo (jana) hapa, yatakwenda katika maeneo yanakohitajika," alisema Sanga.

Meneja mradi wa LTIP, Joseph Shewio alisema magari hayo yamechelewa kununuliwa kutoka na taratibu za ununuzi zilizowekwa na Benki ya Dunia.

Alisema mradi huo una vipengele vinne ikiwamo kupanga matumizi ya ardhi katika ya wilaya, kujenga majengo ya ofisi 25, kunyoosha mipaka ya vijiji, kupanga maeneo ya makaburi na miundombinu mingine.

"Kupitia mradi huu kila mmoja atakuwa na hati yake na hati miliki inatolewa bure. Mwaka huu tumepanga kufikia vijiji 700 hadi sasa tayari tumefikia vijiji 540. Pia tumepanga kufika katika mitaa 660 na halmashauri 36, lakini pia mradi huu hadi sasa umetoa ajira kwa watu zaidi ya 700," alisema.



# Viwavijeshi, panya wawaliza wakulima

Na Dege Masoli, KILINDI

JUMLA ya ekari 7622 za mazao ya mahindi zimevamiwa na wadudu waharibifu aina ya viwavijeshi na kusababisha hasara kwa wakulima wa Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga.

Aidha, panya nao wamevamia mashamba hayo na kuongeza machungu kwa wakulima. Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, iliyosomwa kwenye kikao cha robo ya pili ya Baraza la Madiwani na mwenyekiti wake, Abdalah Ndaro, athari zilizosababishwa na viwavijeshi, pia kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Mbawakavu.

Ndaro ambaye ni Diwani wa Kata ya Mvungwe, alisema kuwa kata 16 zimeathiriwa na janga hilo.

Alisema katika kipindi cha robo ya pili wilaya hiyo imekumbwa na janga lingine la panya waharibifu waliokuwa wakifukua na kula mbegu zilizokuwa zimepandwa mashambani jambo ambalo lilizusha taharuki kwa wakulima wa eneo hilo.

Aidha, alisema jumla ya hekari 1,704 za mahindi ziliokolewa kwa kuwaangamiza panya hao, baada ya zoezi hilo kufanyika katika kata nane zilizovamiwa ambapo halmashauri kupitia idara ya kilimo ilipeleka wataalamu wake mapema kudhibiti hali hiyo.

Kuhusu viwavijeshi, Ndaro alisema tayari idara ya kilimo imeanza kushughulikia tatizo hilo, kwa wataalamu kufika maeneo yaliyokumbwa na uvamizi huo, ili kuona ukubwa wake na kutafuta ufumbuzi.

Ofisa kilimo wa halmashauri ya wilaya hiyo, Seif Sempanga, akizungumza athari zilizotokea, alisema jitihada zimeshafanyika na kwamba lita 7622 za sumu aina ya Profenofos 720EC/ Duduba 400EC/Banafos 720 zimeombwa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania na ufuatiliaji wa maombi hayo unaendelea.

Akizungumzia kuhusu mlipuko wa panya hao, Sempanga alisema lita 58.5 za sumu aina ya Zincphosphide asilimia 80 na kilogramu 348 za chambo (mahindi na pumba) zimetumika katika zoezi hilo la kuwadhibiti wadudu hao, kwenye kata za Songe, Pagwi, Mvungwe, Mabalanga, Mkindi, Jaila, Negero na Kisangasda.




Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Leonard Bandola (kulia), akizungumza kwenye mkutano wa wazazi katika Shule ya Msingi ya Zion, Kijiji cha Mkanyageni, ambapo wameiomba serikali ya mkoa kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) kuweka stendi ndogo ya kusimama mabasi pamoja alama za barabarani katika barabara kuu ya Tanga mjini-Segera. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wazazi wanaowalisha watoto wachanga vyakula waonywa

Na Jaliwason Jasson, MANYARA

WATAALAMU wa lishe, malezi na makuzi ya mtoto mkoani Manyara, wameonya tabia ya wazazi na walezi kuwalisha vyakula watoto chini ya miaka mitano, bila kufuata mpangilio sahihi kwa kuwa itawaletea madhara katika afya na ukuaji wao.

Tahadhari hiyo, ilitolewa jana na Ofisa Lishe wa Mkoa, Januari Dalushi, wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na umuhimu wa vyakula vya nyongeza kwa watoto chini ya miaka mitano.

Aidha, Dalushi alisema mtoto anatakiwa kulishwa makundi sita ya vyakula ambapo kila kundi liwe na aina moja ya chakula cha kundi husika.

Aliyataja makundi ya vyakula hivyo kuwa ni kundi la kwanza ni nafaka, mizizi na ndizi, vyakula vya asili ya wanyama, mikunde, mboga, matunda na kundi la mwisho ni mafuta, ukari na asali ambapo alisisitiza kutumia sukari, asali na mafuta kwa uchache kwa kuwa vinapoteza ladha ya kula kwa watoto.

Aidha, alisema ulishaji wa watoto unatakiwa kuanzia na miezi sita wakipewa uji wapewe vijiko viwili mpaka vitatu kwa siku na asipewe kabla ya kunyonya.

"Mtoto wa miezi saba mpaka nane ale milo mitatu kwa siku na uji apewe kikombe kidogo cha robo kilogramu kisijae,"alisema Dalushi.

Mtaalamu huyo, alisema watoto wa miezi tisa mpaka 11 wale milo mitatu kwa siku na asusa moja yaani milo midogo midogo yenye manufaa kilishe mfano kumpa maziwa, sharubati au karanga," alisema.

Hata hivyo, alisema watoto wa miezi 12 mpaka miezi 24 wapewe vyakula vinavyoliwa na familia na angalau asusa mbili na wanywe kikombe cha robo kilogramu ya uji.

Ofisa lishe huyo alisema mama au baba wanapotoka kazini wawaletee watoto sharubati ya embe na sio embe bali yenye ladha ya embe tu kwa kuwa hakujawahi kuwepo na maembe mengi kiasi hicho.

Alisema watoto wakijaziwa vyakula vya viwandani vitachangia kuwaharibu kiafya hivyo havishauriwi na wataalamu.

Dalushi alisema watoto ambao wanapewa vyakula vya nyongeza wanategemea wakienda kliniki kwa mwezi waongezeke uzito gramu 500 hivyo kama haongezeki uzito kunatokana na kutokulishwa vizuri.

Mshauri wa Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka, alisema lishe bora kwa watoto ndio inawasaidia ukuaji wa ubongo na wasipopewa wakiwa na miaka miwili mpaka mitatu hatakua vizuri.

Vilevile, Gisuka alisema hata wakienda shule uwezekano wa kufanya vizuri darasani utakuwa ni mgumu.

Mkazi wa Mtaa wa Hangoni, Mwajuma Ally, alisema wazazi wengi wamekuwa wakiwapatia watoto wao vyakula vya viwandani ikiwamo shalubati, pipi na sukari ili waache kulia.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) ya mwaka 2021/22-2025/26 na asilimia 92 ya watoto wenye miezi sita hadi nane walianzishiwa vyakula vya ziada kwa wakati unaofaa.

## DC ataka h'shauri kuongeza nidhamu matumizi fedha

Na Dege Masoli, KILINDI

MKUU wa Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Hashim Mgandilwa, ameitaka halmashauri ya wilaya hiyo kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kudhibiti mianya ya ufujaji wa mapato ili kutekeleza lengo la serikali la kuhudumia wananchi.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, Mgandilwa alisema licha ya kulipongeza baraza hilo kwa kukusanya mapato zaidi ya asilimia 50 kwa lengo lililowekwa kwa robo ya pili ya Oktoba hadi Desemba 2023, ilitakiwa kuepuka matumizi yasiyokuwa ya lazima.

"Pongezi hizi ziende sambamba na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, haitakuwa na maana endapo mnakusanya zaidi na kutumia zaidi…tujenge nidhamu ya fedha," alisisitiza Mgandilwa.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Wilaya, aliwaagiza Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA), kuhakikisha makandarasi wanarudi kwenye miradi inayotekelezwa, ili kazi ziendelee na kurejesha mawasiliano ya barabara ambazo zimekuwa kero kwa wananchi kutokana na miundombinu kuharibiwa na mvua.


"TARURA, makandarasi wote warudi kwenye miradi wanayoitekeleza kwa kuwa hali ya hewa siyo mbaya kwa sasa…msisingizie mvua, tumieni kijua kinachowaka kurudisha huduma hasa katika maeneo ambayo yalikuwa hayapitiki kabisa," alieleza.

Hata hivyo, alisikitishwa na kasi ndogo ya wanafunzi kuripoti shule kwa kuwa alisema asilimia 30 ya wanafunzi wa sekondari waliotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza hawajulikani walipo na asilimia 60 ya waliotakiwa kujiunga na shule za msingi hivyo aliagiza viongozi, wazazi na jamii kwa ujumla kuhakikisha watoto hao wanakwenda shuleni.

Katika hatua nyingine, aliwataka viongozi wa serikali za vijiji na wananchi waliopo katika mipaka ya wilaya hiyo na Kiteto mkoani Manyara, kuridhia uwekaji wa alama za mipaka kwenye maeneo yao.

Alisema katika zoezi hilo, pamoja na mambo mengine, lakini kuna machungu yatakayojitokeza hivyo hakuna budi kuyavumilia kama wanavyoweza kufurahia matamu na alisema kunakukosa na kupata kwa hiyo yote wayakubali.

"Katika zoezi hili kunakukosa na kupata sasa yote kuyapokee kwa maslahi ya wengi na hiyo ndiyo tamu na chungu ya uwekaji alama za mipaka kwenye maeneo yetu," alisema.





# Kamati ya Bunge yataka tathmini waathirika wa bwawa la Mwadui

**Na Marco Maduhu,**
KISHAPU

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Nishati na Madini imeitaka serikali kufanya mapitio ya tathmini ya eneo la madhara pamoja na mchakato wa ulipwaji fidia kwa waathirika wa kubomokewa na bwawa la kuhifadhia majitope la mgodi wa Almasi Mwadui Wiliamson Diamond Limited (WDL), uliopo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Shabani Ng'enda, alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea kukagua bwawa jipya liliojengwa na kusema hatua hiyo itasaidia kuondoa mang'uniko kwa baadhi ya wananchi ambao wanaonekana kutoridhishwa na ulipwaji wa fidia kwa kupewa majibu na elimu namna fidia ilivyofanyika.

Pia alisema kamati hiyo inaitaka Wizara ya Madini kusimamia suala la mgodi kuwajibika kwa jamii (CSR), ili kiwango kinachotolewa kilingane na uzalishaji wa almasi licha ya kwamba wanafanya vizuri kwenye eneo hilo, pamoja na kuharakisha mchakato wa kuongeza asilimia ya serikali kumiliki mgodi huo kutoka 25 hadi 37.

"Kwanza nitoe pole kwa Watanzania ambao walipatwa na janga hilo baada ya bwawa la majitope kubomoka, lakini niupongeze mgodi kwa kuwajali wananchi hao ikiwamo kuwapatia huduma mbalimbali za kijamii," alisema Ng'enda.

Vilevile, aliutaka mgodi huo kufanya marekebisho kwenye nyumba ambazo wananchi wamelipwa fidia kwa kuziongezea milango ili iwe miwili kwa ajili ya dharura.

Mhandisi Mkuu wa Mgodi huo, Mipawa Shaghembe, akimwakilisha meneja wa mgodi alisema kwa sasa wanaendelea kufanya uchunguzi wa kisayansi, ili kubaini chanzo halisi cha kubomoka bwawa hilo.

Alisema tangu kutokea kwa tukio hilo, licha ya tume nyingi kufanya uchunguzi juu ya kubomoka kwa bwawa hilo na wao wameamua kufanya uchunguzi wa kisayansi na siyo wa macho tu, ili kubaini chanzo halisi cha kubomoka kwa bwawa hilo ni kipi, ili wachukue tahadhari katika bwawa jipya ambalo wanalitumia kwa sasa.

"Baada ya kumaliza kufanya uchunguzi bwawa hili tunalifunga kabisa na haliwezi kutumika tena katika shughuli zetu za uzalishaji almasi," alisema Mipawa. Alisema katika bwawa jipya la kuhifadhia majitope ambalo wanalitumia kwa sasa, ukaguzi unaendelea mara kwa mara ikiwa ni sehemu ya kuchukua tahadhari, licha ya kwamba limejengwa imara ili kusije tokea madhara tena.

Novemba 7, mwaka 2022 majira ya saa 3 asubuhi bwawa la kuhifadhi majitope la mgodi huo lilibomoka kingo zake na kisha tope kutiririka kwenye makazi ya watu na kuleta madhara makubwa, ikiwamo kufunika nyumba, mashamba, visima vya maji lakini hapakutokea vifo.

Ofisa Mahusiano wa Mgodi huo, Benard Mihayo, alisema ulipwaji fidia wananchi wameshafanyika, pamoja na wengine kuishi kwenye nyumba zao na kusalia watu wanne, ambao wamegoma kujengewa nyumba wakitaka walipewa fidia ya pesa na kwamba taratibu zinaendelea ili walipwe haki yao.



Mhandisi Mkuu wa Mgodi wa Almasi wa Mwadui, Shaghembe Mipawa, akiwaonyesha Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Nishati na Madini bwawa jipya la kuhifadhia majitope la mgodi huo, ambalo kwa sasa wanalitumia katika shughuli za uzalishaji almasi baada ya lile la mwanzoni kubomoka kingo zake. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Watoto 98,000 wapatiwa chanjo ya surua, rubella

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

ZAIDI ya watoto 98,000 wenye umri wa miezi tisa hadi 59 wamekadiliwa kupatiwa chanjo ya ugonjwa wa surua na rubella katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kukabiliana na magonjwa hayo.

Chanjo hiyo ambayo imetolewa kufuatia operesheni ya siku tatu kuanzia Februari 15 hadi 18 imetajwa kukumbana na vikwazo mbalimbali, ikiwamo uvumi unaoitaja chanjo hiyo kuwa na madhara kwa watoto hali ambayo siyo sahihi.

Akizungumza na Kamati ya Afya ya Msingi Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliwataka viongozi wa dini na serikali kuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu na kukanusha uvumi huo wenye nia ovu na upotoshaji.

Alisema kumekuwa na baadhi ya watu wenye nia mbaya ambao wamekuwa wakipotosha juu ya usahihi wa chanjo mbalimbali zitolewazo na serikali zikitajwa kusababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo surua na hatimaye vifo vya watoto.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Fredrick Mugarula, alisema ugonjwa ya surua na rubella huambukizwa kwa njia ya hewa hivyo lengo la kutoa chanjo hiyo ni kuzuia kuenea kwa magonjwa hayo pamoja na kuongeza kinga kwa walengwa hata kama wamewahi kupata chanjo katika utaratibu wa kawaida wa utoaji wa chanjo.

Dk. Mugarula alisema ugonjwa wa rubella unapompata mama mjamzito anaweza kujifungua mtoto mwenye tatizo la ukiziwi, upofu, ugonjwa wa moyo na ukuaji duni kiakili na kimwili hivyo kuitaka jamii kutokupuuza chanjo hiyo.

# Uandikishwaji darasa la kwanza Tarime wasuasua

**Na Timothy Itembe,** TARIME

HALI ya wanafunzi kuandikishwa na kuripoti shule kwa ajili ya kuanza masomo ya darasa la kwanza na kidato cha kwanza wilayani Tarime mkoani Mara imetajwa kuendelea kusuasua, huku viongozi mbalimbali wakitakiwa kuongeza nguvu katika kuhimiza utekelezaji wa suala hilo.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Michael Mtenjele, katika Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Tarime na kusema suala hilo linazidi kusuasua hivyo linahitaji kuongezewa nguvu na viongozi wa ngazi mbalimbali.

"Tunaomba viongozi hususani madiwani kuendelea kufuatilia suala hili ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa elimu kwa mtoto, ikiwa ni sambamba na kuwahimiza wanafunzi kuendelea na masomo kama iliyokusudiwa," alisema Mtenjele.

Alitaja kuzuka kwa wimbi la utoro kwa wanafunzi inayosababisha kushindwa kumudu masomo katika ngazi mbalimbali za kielimu na kuwaomba viongozi kushiriki katika kukomesha matukio hayo na kuwata kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaoshiriki kukwamisha suala hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, alisema hatua hiyo ni muhimu katika katika kusimamia na kupambana kuondoa aibu ya gharama ya watoto kuwa wajinga.

Aidha, baraza hilo lilipitisha bajeti ya utekelezaji wa miradi ya zaidi ya Sh. bilioni 28.9 ikiwamo uendeshaji wa shughuli za ofisi mishahara na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu, Victor Magafu, aliomba kuidhinishiwa na kutumia zaidi ya Sh.bilioni 9.14 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 1.23 ni kutokana na asilimia 40 ya mapato yasiyolindwa ya halmashauri (own Sctwce dev) na Sh.bilioni 7.9 ni fedha ya kutoka serikali kuu na wahisani mbalimbali wa maendeleo.

Baadhi ya madiwani akiwamo Chacha Marwa wa Kata ya Turwa alisema wanafunzi waliandikishwa kuanza darasa la awali, la kwanza na kidato cha kwanza wanatakiwa kwenda kuripoti shuleni kuanza masomo kwa kuwa serikali imeondoa michango iliyokuwa ni kikwazo kwa wanafunzi kuandikishwa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 20, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**China na vituko vya kumaliza punda Afrika**



Ukurasa 12

Wanafunzi 49,000 mikoa hii kupata madarasa, mabweni ya kisasa ni wa msingi na sekondari



Ukurasa 13

Wazazi jueni simu janja, TV vinawaangamiza watoto wenu

SAYANSI

NA JANE MATHIAS

## HILI LILIFANIKIWA

# Kupikia mkaa na kuni sasa basi mgunduzi aibuka na jiko la maji

MWANASAYANSI asiyesikika, George Rubagumya maarufu Bwemelo, kazi zake za ubunifu na ugunduzi kwa mara nyingine zinathibitisha usemi kuwa hawavumi lakini wamo.

Rubagumya mkazi wa Segerea Dar es Salaam, ameanza kutikisha anga za ubunifu na ugunduzi kwa muda mrefu, akianzia kuunda mtambo unaotumia maji kidogo ya kisima kuzalisha umeme wa megawati 42,000.

Ni mambo yanayoibuka katika mahojiano na Nipashe yanayofanyika nyumbani kwake hivi karibuni.

Bwemelo anafafanua kuwa kiasi hicho cha nishati chenye megawati 42,000 ni umeme unaweza kutosha nyumba 25 za watu wenye kipato cha kati wanaotumia friji, televisheni, pasi na kuwasha taa.

Anaongeza kuwa kwa wenye nyumba za umeme mkubwa mfano wanaofua na mashine, wenye 'deep frizer', viyoyozi, wanaopikia umeme na kutumia vifaa vingi vikubwa megawati 42,000 zinatumiwa na nyumba 12.

Anasema mtambo sasa unatakiwa kufanyiwa majaribio na kuboreshwa ili kutumiwa na kuandaliwa kufikia kiwango kinachotakiwa na kuzalisha umeme bila kukoma au endelevu, ukizimwa hauwashwi kwa muda mrefu.



George Rubagumya au Bwemelo, akiwa kazini . **PICHA: JANE MATHIAS**

Mwalimu Rubagumya anasema ili kufanikisha uwekezaji huo anahitaji Shilingi milioni 12. Akisema hadi sasa ametumia takribani milioni 5 kutengeneza mitambo ya umeme huo wa maji ikiwa ni gharama za kununua vifaa mbalimbali.

Anasema ameufanyia majaribio mtambo huo kuzalisha nishati jadidifu na unaweza kutumika kupunguza tatizo la umeme na sasa amekuja na jambo jingine.

### KUPIKIA MAJI

'Bwemero' akizungumzia jambo jipya anasema ni teknolojia ya kutumia maji kupikia badala ya kung'ang'ania kuni, mkaa, gesi na nishati nyingine.

Rubagumya anasema kuwa katika utafiti wake amebaini kuwa mbali na maji kutumika kuzalisha nishati ambayo ni umeme wa maji, yanaweza pia kuwa moto ukapika chakula na kukiivisha.

"Majaribio yamefanyika na kupata mafanikio makubwa, ni jambo la kujivunia sana kwa Mtanzania kugundua maji yanaweza kupika kama ilivyo kwa nishati ya gesi," anasema.

Anaongeza kuwa maji yana viambato au compound za mchanganyiko wa oxygen na hydrogen ($H_2O$).

Kwa mujibu wa Bwemelo kinachofanya uweze kupika kwa kutumia maji ni uwepo wa hydrogen kwa sababu ndiyo inayowaka.

Anasema katika utafiti wake, ameunda mtungi unaweza kuchakata na kutenga maji na viambato vingine kwa kuyavunja kitaalamu na kupata hydrogen inayowaka na kupika.

Anafafanua kuwa mpishi anaweka maji kwenye mtungi maalumu kama ambavyo unatumia jiko la 'Mchina' kupika.

"Mtungi huu una uwezo wa kuvunja maji na kupata hydogen na oksejeni. Nikumbushe maji yanaweza kutengwa na kwa kutumia mkondo mnyoofu wa umeme na kuwekwa tindikali ya sulphuric acid kidogo kwenye chombo maalum," anasema.

Anafafanua kuwa mkondo mnyoofu ni umeme unaotoka kwenye betrii ya umeme ya simu au ya gari inayounganishwa na nyaya na kuwekwa kwenye maji na huko hydrogen hujitenga na oksijen, na kwenye kupata moto inawekewa kitu kingine kuilinda isilipuke sababu inashika moto.

Anasema hewa hiyo inawaka kwa kiwango cha kadri na moto wake ni wa rangi ya bluu kama wa gesi asilia au ya mitungi.

"Inawaka kwa moto wa bluu kama gesi unavyoiona. Pia hydrogen inatumika palepale unapoizalisha, siyo kuhifadhi kwenye mitungi kama wanavyofanya kwenye gesi kwani inaweza lipuka," anasema Bwemelo.

Anaongeza kuwa baada ya kukamilisha mapishi, mtumiaji anazima kwenye mkondo mnyoofu wa umeme wa betrii na kisha kuwasha tena sehemu hiyo kwa ajili ya kuendelea kupika na kwamba betrii 'inayokonekti' nyaya hizi inaingia kwenye maji na kuvunjavunja viambato.

Anasema katika teknolojia yake hiyo, kuna vifaa vingi ambavyo vinafanikisha kuhimili presha au msukumo wa hewa hiyo ya hdrogen ili kuilinda isilipuke na kupikia kwa kadri inavyohitajika.

Anasema hydrogen inayopatikana inapita kwenye mrija au mpira kwenda kwenye jiko lenye 'banner' mbili kama yalivyo ya gesi au umeme.

"Majiko haya ya gesi yaliyoko mtaani ninayabadilisha mfumo wake kuruhusu hydrogen iingie na kuwaka katika kiwango chake bila kulipuka."

### FAIDA

Bwemero anataja faida ya kutumia nishati maji kupikia kuwa ni pamoja na kuboresha mazingira kwa sababu inavunja maji na kupata oxygen ambayo inatumika kupumua na kuishi kwa kuvuta na kupumua hydrogen ikivunjwa na kwamba ikipoa inarudi kuwa mvuke ambao ukipoa yanakuwa maji.

Anasema nishati yake hiyo ni bei nafuu ikilinganishwa na gharama kubwa ya gesi asilia ya kwenye mitungi inayotoka

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# Wanafunzi 49,000 mikoa hii kupata madarasa, mabweni ya kisasa ni wa msingi na sekondari



Baadhi ya madarasa ya kisasa yaliyojengwa na serikali hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

SEKTA ya elimu ni eneo ambalo Tanzania inaliwekea mkazo ili watoto wenye umri unaostahili kuwa darasani waende shule, lakini pia wasome kwenye mazingira bora yanayowaongezea ari ya kutamani kusoma na kuelimika.

Katika kufanikisha mikakati hiyo na malengo kutimizwa wadau mbalimbali wa maendeleo wamekuwa wakijitolea kuchangia katika sekta ya elimu kwa kujenga miundombinu na kutoa misaada kupitia fedha za Corporate Social Responsibility (CRS).

Katika juhudi za kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundisha, kampuni za Barrick inayochimba dhahabu kwa ubia na kampuni ya serikali ya Twiga Mineral Cooperation wanaomiliki kwa pamoja migodi ya Bulyanhulu mkoani Shinyanga na Barrick North Mara uliopo Mara, mwaka 2023 unapomalizika zimekamilisha ujenzi wa madarasa 396.

Pamoja na madarasa yapo mabweni yatakayonufaisha mikoa ya Shinyanga, Mara, Geita, Arusha na Mbeya ambapo ujenzi wa madarasa umeshuhudiwa kwenye baadhi ya wilaya, anasema Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow.

Katika ripoti ya robo ya mwisho ya mwaka 2023, Dk.Bristow anatangaza kutumia zaidi ya Shilingi bilioni 25 kujenga madarasa 396 na mabweni 97 katika awamu ya kwanza ya mpango wa kuboresha miundombinu ya elimu.

Aidha, kampuni imepanga kutumia dola milioni 30 (zaidi ya Shilingi bilioni 65) kuunga mkono juhudi za serikali kuboresha sekta ya elimu ambapo migodi hiyo imepanga kujenga vyumba vya madarasa 1,090 na mabweni 270 katika mikoa mbalimbali.

Akizungumza wakati anawasilisha ripoti kwenye mkutano unaozishirikisha kampuni hizo, Wizara ya Madini na viongozi wa mikoa ya Shinyanga, Mara na Geita, anasema programu hiyo itanufaisha wanafunzi 49,000 wa msingi na sekondari.

"Hii ni katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha miundombinu ya elimu na nia ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuboresha sekta ya elimu Tanzania." Anaongeza:

"Elimu ndiyo msingi wa kila kitu, tunaamini katika elimu tutapata wataalamu wengi zaidi sio tu kwenye sekta ya madini lakini na sekta nyingine, kwetu ni fahari kusaidia sekta hii muhimu na kuunga mkono juhudi za serikali," anasema Bristow.

Anawaambia wajumbe katika taarifa yake hiyo kuwa mpaka kufikia Desemba mwaka jana dola milioni 8.06 sawa na Shilingi bilioni 19.9 zilikuwa zimetumika katika ujenzi wa madarasa na mabweni hayo.

Katika mkakati huo wa ujenzi wa madarasa na mabweni, wanafunzi 49,000 watanufaika hatua inayosifiwa na wazazi na walezi akiwamo mkazi wa Kahama, Josephat Masanja, akisema sehemu kubwa wanafunzi wa wilayani Kahama wanafaidika na uboreshwaji wa miundombinu ya shule.

"Sasa hivi kwenye maeneo yetu tuna shule zenye ubora, uwepo wa migodi hii umesaidia tunaweza kupeleka watoto wetu shule za bweni," anasema Masanja.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Hyasinta Bundala ambaye anasema wanatarajia hata ufaulu wa wanafunzi utaongezeka kutokana na kuboresha miundombinu shuleni .

"Tunaomba ushirikiano uliopo kati ya serikali na migodi ya Barrick uendelee, kutokuwapo kwa miundo mbinu bora ni chanzo cha wanafunzi kutofanya vizuri, lakini kwa sasa katika maeneo ambayo ujenzi wa madarasa na mabweni unafanyika hali itakuwa tofauti," anaongeza Hyasinta.

Katika ujenzi wa madarasa na mabweni hayo, Dk. Bristow anasema hayajengwi kwenye mikoa yenye migodi peke bali ni kwenye sehemu mbalimbali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Katika ushirikiano wetu na TAMISEMI, Barrick inatoa makandarasi wa ujenzi ili kupata ubora katika miundombinu tunayojenga na kufanya mradi huu kuwa wenye tija zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akizungumzia juhudi hizo anasema migodi hiyo ya Barrick imekuwa msaada mkubwa katika kuisaidia serikali kuleta maendeleo ya sekta mbalimbali.

Anaongeza kuwa ukiondoa ujenzi wa madarasa na mabweni mkoani Shinyanga na maeneo mengine, pia wamefanikisha ujenzi wa jengo la kisasa la uwanja wa ndege wa Kahama.

"Serikali ya mkoa tunaona juhudi za wenzetu katika kuhakikisha wananchi wanafaidika na uwepo wa migodi hii, mwaka jana wilaya ya Msalala ilipokea Shilingi bilioni 1.9 fedha za mradi wa maendeleo kwa jamii inayozunguka mgodi wa Bulyanhulu ambayo inatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo," anasema Christina.

Aidha, anaahidi kushirikiana na mgodi huo katika maeneo mbalimbali kuhakikisha kila mmoja anafaidika na uwepo wa dhahabu na hilo ndilo lengo hasa la serikali yetu akisema inataka kuona uwepo wa migodi ukinufaisha Watanzania na kuchangia maendeleo ya nchi.

Naibu Waziri wa Madini, Stevin Kiruswa, anakizungumzia juhudi hizo, anasema migodi inafanya makubwa kusaidia jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo na kufaidika kuwepo kwa migodi hiyo.

Anasema uwepo wa programu ya ujenzi wa madarasa zaidi ya 1,000 ni jambo ambalo litaacha kumbukumbu hata migodi hiyo itakapomaliza muda wake.

"Lengo la serikali ni kuona uwepo wa migodi hapa nchini inawanufaisha wananchi sasa wenzetu wa Barrick wanalitekeleza hili kwa miradi yao mbalimbali wanayoianzisha na kuitekeleza ikiwamo programu hii ya kuboresha miundombinu ya elimu," anasema Kiruswa.

Kuhusu kukamilika kwa programu hiyo ya ujenzi wa madarasa, mabweni na matundu ya vyoo, Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Bristow, anasema awamu ya pili ya programu hiyo inatarajiwa kuanza wakati wowote kufikia ahadi ya ujenzi wa madarasa 1,090 na mabweni 270.

## Kupikia mkaa na kuni sasa basi mgunduzi aibuka na jiko la maji

**INATOKA UK.11**

kwenye mafuta na kwa kuvunwa ardhini.

"Watu wengi wanaweza kutumia kwa sababu ni bei rahisi na kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni na kutunza na kulinda mazingira," anasema mbobezi huyo wa sayansi.

Anasema teknolojia hiyo na ile ya umeme wa maporomoko ya maji alibuni pamoja na kuamua kuanza na kimoja kisha kufuata kingine baada ya kuonyesha mafanikio.

**HISTORIA**

Mwalimu Rubagumya ana tatizo la macho akilipata mwaka 2014 na kutafuta matibabu kwenye hospitali mbalimbali ikiwamo Muhimbili na kuthibitika kuwa ana presha ya macho au 'glycoma'.

Kabla ya hapo alikuwa mwalimu wa fizikia na hesabu akifundisha sekondari. Anasema amekuwa na mikwamo ukiwamo wa kushindwa kumaliza shahada ya uhandisi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Nilikuwa mwaka wa nne nikisoma electrical engineering- uhandisi wa umeme. Niliumwa malaria kali ikapanda kichwani nikashindwa kufanya mitihani ya kurudia nilikuwa Na'suplimentary', nikafukuzwa kwa kwa sababu hiyo. Hata niliowatuma kuwa ninaumwa hawakufikisha taarifa," anaeleza kuwa hayo yalitokea mwaka 2000 na hajapata tena nafasi ya kusoma zaidi.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wazazi jueni simu janja, TV vinawaangamiza watoto wenu

• Hugeuzwa waraibu, waathirika wa unyanyasaji mitandaoni



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alipofungua mafunzo kuhusu athari za mitandao kwa watoto. Kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Watoto, Mathias Haule, kulia ni mtaalamu wa ulinzi na usalama wa mtoto kutoka UNICEF, Joseph Matimbwi. **PICHA: SABATO KASIKA**

KATIKA dunia ya sasa ambayo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ndiyo injini inayoendesha shughuli karibu zote, si ajabu kukuta watoto wakitumia mitandao ya kijamii kuanzia facebook hadi tiktok.

Wakati mitandao hiyo ikiwezesha kujifunza, kuvumbua, kubuni vitu mbalimbali na kuwasiliana na wenzao, inawaweka kwenye hatari ya kupata madhara ya ukatili wa mtandaoni, kuwakwaza na kuharibu hatima zao kutokana na kushirikishwa maudhui yanayopotosha.

Kutokana na mazingira hayo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Makundi Maalumu inakusudia kuweka mkakati wa kudhibiti athari za mitandaoni kwa watoto, anasema Waziri Dk. Dorothy Gwajima.

Ikianza na kutoa elimu ya uelewa wa ukatili huo kwa wazazi, walezi na walimu na pia kufanya mapitio ya sheria na kanuni itakayofanikisha kudhibiti ukatili wa watoto mtandaoni, anaongeza.

Aidha, maudhui yasiyofaa lazima kudhibitiwa yasimfikie mtoto na kwamba wazazi na walezi wanatakiwa kutimiza wajibu wa kufuatilia vifaa vya kielektroniki wanavyotumia watoto wao.

Pia kuwawekea muda maalumu wa kuvitumia, kwa vile zipo taarifa kuwa wengine hawalali wamekuwa waraibu, wanakesha wakichati na hata kuangalia maudhui yasiyofaa na yanayowaangamiza.

Pia, wapo wanaokataa shule wakijiingiza katika makundi ya mtandaoni yenye maadili yasiyofaa pasipo mzazi au mlezi kufahamu.

Aidha, Waziri anasema tayari wamezindua kampeni ya Usalama wa Mtoto Mtandaoni na uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Taifa ya Usalama wa Watoto Mtandaoni itakakayoongoza kampeni hizo.

"Kaulimbiu inaitwa 'usalama wa mtoto mtandaoni ni jukumu letu chukua hatua', hivyo, tutazungumza nchi nzima kuelimisha jamii na viongozi wao kuanzia ngazi ya chini na walimu pia ili wawasaidie wanafunzi kuepuka ukatili mtandaoni," anasema.

Ni katika mafunzo yanayofanyika jijini Dar es Salaam kuhusu mafunzo ya usalama wa mtoto mtandaoni kwa wahariri na waandishi wa vyombo vya habari.

Waziri anafafanua kuwa TEHAMA, inakwenda kwa kasi na maudhui yanayosambaa mtandaoni ni hatari kwa watoto.

"Tumeona sasa kuna haja kuwa na mkakati wa kufanya mapitio ya sheria na kanuni, kutoa elimu kwa wazazi na walezi kwani wamejisahau na kuwapa watoto hao vifaa vya kielektroniki zikiwamo simu, kompyuta na televisheni pasipo kuwa karibu nao kujua nini wanakitazama na kujikuta wakirubuniwa au kufanyiwa ukatili kupitia mtandao," anasema Dk. Dorothy.

Waziri anataja changamoto nyingine zinazowakumba watoto mtandaoni kuwa ni udhalilishaji wa kingono, uraibu wa mtandao unaowafanya waache mambo mengine kutokana na kukaa kwa muda mrefu mtandaoni.

> "Ingawa kuna faida nyingi kutumia mitandao, athari zinazowakuta watoto katika hayo matumizi hayo bila uangalizi wa karibu zinajumuisha kuanza ngono katika umri mdogo hivyo kupata athari za kisaikolojia na mmomonyoko wa maadili kutokana na mwingiliano wa mila na desturi za mataifa mengine ikiwamo kuiga ushoga na usagaji," anasema.

**TAARIFA KITAFITI**

Anaongeza kuwa utafiti unaofanywa mwaka 2022 na wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Tanzania, unaonyesha kuwa watoto wa miaka 12 hadi 17, karibu asilimia 67 wanatumia mitandao maarufu ambayo ni facebook, X (zamani twitter), instagram, whatsap, tiktok na telegram, huku asilimia nne ya watoto wanaotumia mitandao wakiathiriwa na aina tofauti za ukatili.

Waziri Dorothy anataja baadhi ya ukatili huo kuwa ni kukutana na wahalifu waliwasiliana nao, huku asilimia tano ya watoto waliotumia mitandao, walishawishiwa au kulazimishwa kutuma picha zao za utupu.

"Ingawa kuna faida nyingi kutumia mitandao, athari zinazowakuta watoto katika hayo matumizi hayo bila uangalizi wa karibu zinajumuisha kuanza ngono katika umri mdogo hivyo kupata athari za kisaikolojia na mmomonyoko wa maadili kutokana na mwingiliano wa mila na desturi za mataifa mengine ikiwamo kuiga ushoga na usagaji," anasema.

Kwa mujibu wa waziri, kumekuwapo na jitihada mbalimbali za kisera na kisheria za kimataifa, kikanda na kitaifa katika kuwalinda watoto na vijana balehe dhidi ya ukatili wa mitandaoni zikiwamo Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya 1998 kifungu cha 12.

Aidha, anataja vifungu vingine vya 12 na 13 vya kanuni za maudhui mitandaoni, 2018 chini ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, ya 2015 na vifungu vya 83 na 158 (1) na (b) vya Sheria ya Mtoto ya 2009.

"Elimu ya uelewa kuhusu ukatili wa mtoto mtandaoni namna ya kujilinda na pia kufanya mapitio ya sheria na kanuni, vitasaidia mtoto anapotumia vifaa vya teknolojia akiwa salama ili tutengeneze kizazi kilicho bora na salama kinachotegemewa miaka ya usoni," anasema.

**WANA HAKI, LAKINI**

Mtaalamu na mshauri wa masuala ya usalama mtandaoni na uchunguzi wa makosa ya kidigitali kutoka kitengo cha Africa Information and Communicaton Technologies Alliance (AFICTA) cha Dar es Salaam, Yusuph Kileo, anasema, mtoto haizuliwi kutumia teknolojia lakini lazima elimu itolewe ili kuwa na matumizi sahihi ya mitandao.

Kileo anasema, dunia ilivyo sasa mtoto mdogo anaweza kuwasha simu akatafuta kile anachokihitaji ikiwamo katuni na kwamba baadhi ya nchi zilipogundua hilo zimeanza kuchukua hatua za kuwalinda.

"Hata sisi Tanzania hatujabaki nyuma, tuna mikakati kama aliyotaja waziri ikiwamo ya kuongezea nguvu sheria na taratibu ili kuwalinda watoto dhidi ya ukatili mtandaoni," anasema Kileo.

Anawataka wazazi na walezi ambao wamezoea kuwapa watoto simu bila kujua nini wanachokizatama mtandaoni wawe makini kwa kuwaelimisha watoto umuhimu wa matumizi sahihi ya simu.

"Ni vyema mzazi au mlezi asimwachie mtoto wake simu au kifaa cha kielektroniki kama hujui nini anakwenda kukitazama, hivyo, ingekuwa vizuri mtoto asipewe kwani utakuwa umemsaidia, ataelekeza akili zake kwenye masomo shuleni," anasema.

Mtafiti wa saikolojia ya makuzi na elimu kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Heziron Onditi, anasema, utandawazi haukwepeki, lakini umakini katika matumizi ya vifaa vya kielektroniki ni ya muhimu.

Onditi, anasema, utandawazi haukwepeki, lakini umakini katika matumizi ya vifaa vya kielektroniki ni ya muhimu.

Anasema, kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, watumiaji wa simu walikuwa wamefikia watu milioni 70.03, na kwamba taarifa hiyo inaonyesha kuwa Watanzania wengi wanatumia simu.

"Jambo la kuzingatia ni matumizi sahihi na muda sahihi wa kutumia vifaa hivyo, badala ya kuacha mtoto anashinda akiperuzi simu au kompyuta, kuwaacha wakifanya hivyo si sahihi," anasema Onditi.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# China na vituko vya kumaliza punda Afrika

## • Ngozi yake huzalisha dawa kukomesha uzee



PUNDA huibwa katika sehemu nyingi za Afrika na maeneo mengine duniani ambayo yana idadi kubwa ya wanyama kazi hao.

Ni biashara yenye utata ya kimataifa ya ngozi ya punda inayotumiwa kuzalisha tiba iitwayo Ejiao.

Kenya ni miongoni mwa nchi ambazo wizi wa punda unatikisa wakipelekwa China ambako dawa ya jadi inayotengenezwa na protini na madini ya 'amino acid (gelatin), kutoka kwenye ya punda inahitajika kila leo.

Ejiao, inaaminika kuwa inaimarisha afya na kupunguza kuzeeka na pia kumfanya mtumiaji kuwa kijana zaidi.

Ngozi za punda huchemshwa kutoa gelatin, ambayo hutengenezwa kuwa unga au poda, vidonge au kimiminika au huongezwa kwenye chakula.

Katika ripoti mpya ya Hifadhi ya Punda, ambayo imefanya kampeni dhidi ya biashara hiyo tangu 2017, inakadiria kuwa duniani kote punda milioni 5.9 huchinjwa kila mwaka ili kupata dawa hiyo.

Na shirika hilo linasema kuwa mahitaji yanaongezeka, ingawa haikuwezekana kuthibitisha takwimu hizo kutoka vyanzo vya kuaminika.

Barani Afrika, ambako karibu theluthi mbili ya punda milioni 53 duniani wanaishi, kuna sheria kadhaa. Usafirishaji wa ngozi za punda ni halali katika baadhi ya nchi na haramu katika mataifa mengine.

Lakini mahitaji makubwa na bei ya juu ya ngozi huchochea wizi wa punda na Hifadhi ya Punda inasema imegundua wanyama wakihamishwa kuvuka mipaka ya kimataifa ili kufikia maeneo ambayo biashara hiyo ni halali.

Hivi karibuni kunaweza kuwa na mabadiliko kwani serikali nyingi za Afrika na Brazil ziko tayari kushirikiana kupiga marufuku kuchinja na kusafirisha punda ili kukabiliana na ukatili dhidi ya wanyama hao.

Solomon Onyango, anayefanya kazi katika Hifadhi ya Punda mjini Nairobi, anasema:

"Kati ya 2016 na 2019, tunakadiria kuwa karibu nusu ya punda wa Kenya walichinjwa kwa ajili ya biashara ya ngozi."

Hawa ni wanyama wanaobeba watu, bidhaa, maji na chakula uti wa mgongo wa jamii maskini za vijijini.

Kwa hivyo ukubwa na ukuaji wa kasi wa biashara ya ngozi umewatia hofu wanaharakati na wataalamu na kuhamasisha watu wengi nchini Kenya kushiriki katika maandamano ya kupinga biashara ya ngozi ya punda.

Pendekezo la kupiga marufuku mauzo ya punda barani Afrika kwa muda usiojulikana liko kwenye ajenda katika Mkutano wa Wakuu wa Umoja wa Afrika, unaotarajiwa kuwajumuisha viongozi wote wa mataifa uliomalizika Jumapili iliyopita na kwamba itasaidia kuwalinda wanyama hao.

> "Punda ni wanyama asili kwa maisha ya mashambani katika sehemu nyingi za dunia na wana nguvu hutembea hata saa 24 bila kunywa maji na wanaweza kunywa na kurejesha maji kwa haraka bila kupata shida.

"La sivyo kizazi kijacho hakitakuwa na punda," anasema Onyango.

Lakini je, marufuku kote barani Afrika na Brazili inaweza kubadilisha biashara mahali pengine? Wazalishaji wa dawa ya Ejiao walikuwa wakitumia ngozi ya punda kutoka China, lakini, Wizara ya Kilimo na Masuala ya Vijijini ya nchi hiyo, inasema idadi ya punda ilishuka kutoka milioni 11 mwaka 1990 hadi chini ya milioni mbili 2021. Wakati huo huo, Ejiao ambayo ilikuwa kama kipodozi cha kawaida iligeuka na kuwa maarufu kote China, kampuni za Kichina zikitafuta bidhaa za ngozi nje.

Machinjio ya punda yalianzishwa katika sehemu za Afrika, Marekani Kusini na Asia, hilo lilisababisha vuta ni kuvute kuhusu biashara hiyo.

Ethiopia, ambapo ulaji wa nyama ya punda ni mwiko, moja ya machinjio ya punda nchini humo yalifungwa mwaka 2017 kutokana na maandamano ya umma na vilio vya watu na kwenye mitandao ya kijamii.

Wakati Tanzania na Ivory Coast zilipiga marufuku kuchinja na kusafirisha ngozi za punda mwaka 2022, lakini taifa jirani na China ya Pakistan inaikubali biashara hiyo.

Mwishoni mwa mwaka jana, ripoti za vyombo vya habari zilipigia debe taarifa kuhusu "zizi rasmi la punda" la kwanza nchini humo kukuza "baadhi ya mifugo bora", ambayo ni biashara kubwa.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa uhusiano kati ya China na Afrika Profesa Lauren Johnston, kutoka Chuo Kikuu cha Sydney, soko la Ejiao nchini China liliongezeka thamani kutoka takriban Dola bilioni 3.2 mwaka wa 2013 hadi takriban Dola bilioni 7.8 mwaka wa 2020.

Hali hiyo imeleta wasiwasi kwa maofisa wa afya ya umma, wanaharakati wa ustawi wa wanyama na hata wachunguzi wa uhalifu wa kimataifa.

Utafiti umebaini kuwa shehena za ngozi za punda hutumika kusafirisha bidhaa nyingine haramu za wanyamapori.

Kwa viongozi wa mataifa, kuna swali la msingi, je, punda wana thamani zaidi kwa uchumi unaoendelea wakiwa wamekufa au wakiwa hai?

Kama mmoja wa wanaotumia punda anayesema katika jamii yake ya wakulima wadogo na watumia punda huuza bidhaa zao na kupata pesa kwa kuuza maji ili kulipia karo za shule kusomea kozi mbalimbali.

Punda ni wanyama asili kwa maisha ya mashambani katika sehemu nyingi za dunia na wana nguvu hutembea hata saa 24 bila kunywa maji na wanaweza kunywa na kurejesha maji kwa haraka bila kupata shida.

Lakini kwa sifa zao zote, punda hawazaliani kwa urahisi au kwa haraka, kwa hivyo wanaharakati wanahofia kwamba ikiwa biashara haitapunguzwa, idadi ya punda itaendelea kupungua, na kuwanyima watu maskini zaidi njia ya kujikimu kimaisha na kuwanusuru wake zao na kazi ngumu za kubeba mizigo.

Kama Onyango anavyoeleza: "Hatukuwahi kufuga punda wetu kwa ajili ya kuwachinja kwa wingi."

Profesa Johnston anasema punda wamekuwa njia ya usafiri wa maskini kwa millennia nyingi mfano hubeba watoto, wanawake, walimbeba Mariamu alipokuwa na mimba ya Yesu lakini pia walimchukua wakati anaingia Jerusalemu," anasema.

Uchunguzi uliofanywa na National Library of Medicines, uchunguzi uliofanywa kutambua ubora wa Ejiao kwa wagonjwa wenye upungufu wa damu ilithibitika kuwa inaweza kusaidia kuondoa tatizo hilo na kupunguza kizunguzungu.

**BBC**



**HABARI DODOMA**

## Wakulima wataka shamba darasa kujifunza zaidi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, wameomba kampuni ya Intracom Fertilizers Limited inayomiliki viwanda vya kuzalisha mbolea aina ya Fomi kuanzisha mashamba darasa, ili wakulima wapate fursa ya kujifunza matumizi sahihi ya mbolea hiyo.

Wakizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichofanyika mwishoni mwa wiki, walisema mbolea ya Fomi imeonekana kupendwa na wakulima wengi wa Mkoa wa Singida, lakini tatizo wengine wanashindwa kufuata taratibu za namna ya kuitumia kutokana na kutokuwa na elimu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Simon Mapunda, alisema "Ni vizuri mkaanzisha shamba darasa maana sio wakulima wote wanafahamu namna ya kutumia mbolea yenu hii lakini mkiwa na shamba darasa kwa kila kata mtasaidia sana."

Aidha, alisema kampuni hiyo inapaswa kufanya utafiti wa mbolea itakayofaa kwa ajili ya zao la korosho ambalo limeanza kulimwa wilayani humo.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Intracom Fertilizers Limited, Dk. Keneth Masuki, alisema Mkoa wa Singida kwa msimu huu wa kilimo wa 2023/24 umekuwa ni mmoja wa mikoa iliyohamasika sana kutumia mbolea zinazozalishwa na kiwanda kinachomilikiwa na kampuni hiyo.

Masuki alisema kwa takwimu zilizopo katika mfumo wa Mdhibiti Mkuu wa Mbolea Tanzania (TFRA) zaidi ya tani 486 za mbolea zimenunuliwa na wakulima wa mkoa huo kati ya hizo 276 zimeuzwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

"Kiasi kikubwa cha mbolea kinaonekana kimeuzwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa sababu kuna ghala kubwa la kuuzia mbolea ambapo wakulima wengi wanafika hapo kununua," alisema.

Alisema Wilaya ya Mkalama imefanya vizuri katika matumizi ya mbolea hii ni kutokana na kuwepo kwa wakala ambaye amekuwa akisambaza hadi vijiji kwa wakulima.

"Tofauti na matarajio Mkoa wa Singida umefanya vizuri katika mbolea na hili tunamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba ambaye amekuwa akisisitiza matumizi ya mbolea," alisema.

# STAMICO yasaini mkataba uchorongaji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO), limesaini mkataba wa miezi sita wenye thamani ya Sh. bilioni 2.7 kwa ajili ya uchorongaji katika mradi wa Singida Gold Mine.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo mjini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, aliahidi Kampuni ya Shanta Mining kuwapatia huduma bora ya uchorongaji katika mgodi wa Singida Gold Mine.

Alisema tukio hilo ni sehemu ya mageuzi ambayo shirika hilo linaendelea kufanya katika ushiriki wake kwenye mnyororo mzima wa shughuli za uchimbaji na utafiti wa madini.

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa mgodi huo, Mhandisi Honest Mrema, alisema kampuni hiyo imeamua kuingia kandarasi hiyo na STAMICO kwa kuwa wanahitaji mashine za kisasa kwa ajili ya uchimbaji na kuendelea kufanya utafiti katika eneo lao wanalomiliki leseni.

"Lengo leu tunataka kufikia lengo la kuwa mgodi wa kati kwa kuchoronga sana mwaka huu na ujao ili kuupanua mgodi wa dhahabu wa Singida," alisema.

Aliongeza "Kwa historia yenu tuliyosikia hizi mita 5,000 ni za kuanzia tu, tunaweza tukaongeza kiasi kutoka kwenye hizo dola milioni 1.08 na kuwa mara tatu zaidi kutoka na matokeo ya kufanya vizuri kwasababu maeneo tunayo, pia tunaamini huu ushirikiano ni wa muda mrefu sio wa miezi sita tu."

Hivi karibuni alipotembelea mgodi huo, Mavunde aliwataka wamiliki wa migodi nchini kujenga mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka na kuwasaidia kuwainua kiuchumi kwa kununua bidhaa zinazozalishwa na wananchi.



Wajumbe wa Bodi ya Wahariri wa Jarida la Bunge na Maofisa wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ofisi ya Bunge wakiwa katika mafunzo ya kuwajengea uwezo jijini Dodoma jana. Mafunzo hayo ya wiki mbili yamefunguliwa na Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi na Usalama, Mohamed Mwamga, kwa niaba ya Katibu wa Bunge. **PICHA: HALIMA MOLLEL**

# Taka za plastiki zaongoza kuchafua mazingira nchini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

IMEELEZWA kuwa asilimia zaidi ya 60 sawa na tani 318,000 ya taka za plastiki zinazalishwa hapa nchini, hali inayochangia uchafuzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali.

Mkufunzi mwezeshaji wa masuala ya uhifadhi wa mazingira nchini na Andrew Kazura aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa Shirika lisilo la kiserikali la Wated ulioandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Gaia wenye lengo la kudhibiti matumizi ya plastiki.

Alisema kuwa wadau wanatakiwa kuendelea kushirikiana na serikali hasa kwenye udhibiti wa matumizi ya plastiki kutokana na kuzalisha taka nyingi na kuleta uchafuzi wa mazingira kwa baadhi ya maeneo.

Alibainisha kuwa bado jamii ina uelewa mdogo katika udhibiti wa taka ngumu ikiwamo plastiki na kuomba wadau na serikali kuongeza udhibiti wa taka hizo.

Alifafanua zaidi ya kuwa wamekuwa na mafunzo ambayo wamefanya Dar es Salaam na Dodoma, lengo kubwa ni kuwasilisha uelewa wa sera za udhibiti wa taka ngumu hasa plastiki, changamoto zake sera na mapungufu yake, yamechangia kuwaleta wadau pamoja kutoa maoni na mapendekezo juu ya jitihada za pamoja ambazo zitaleta.

Alisema kuwa takwimu za kidunia zinaonesha plastiki ni janga kwani takribani tani milioni nane za plastiki zilizalishwa duniani, kati ya hizo tani milioni 6.3 za taka zinazotokana na plastiki ziliweza kuzalishwa duniani.

"Tunakuwa na hizi takwimu lakini pia kwa nini hali iko kama ilivyo, japo tuna sera lakini suala la utekelezaji unaweza kuwa changamoto kwa baadhi ya maeneo kwani kumekuwa na sera na kanuni.

"Ambazo zinasimamiwa na Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau serikali imefanya jitihada kazi kubwa katika udhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki kupitia kanuni chini ya sheria ya uhifadhi wa mazingira 2004," alisema.

Alisema kumekuwa na jitihada nyingine ya udhibiti wa vifungashio vya plastiki bado kumekuwa na tatizo kutokana na kutumika kama vibebeo.

"Tumewaleta wadau pamoja ili kuja na suluhu ya pamoja ikiwamo kutumia mbinu mbalimbali ambazo kama asasi za kiraia zimeweza kufanya katika ngazi za tawala za mikoa na serikali za mitaa kupitia utoaji wa elimu kwa jamii jinsi ya matumizi, kwani plastiki nyingine zimekuwa zikiokotwa na kupelekwa viwandani kuchakatwa na kuwa bidhaa," alisema. Aliongeza "Hili limekuwa chachu kama nchi tutakuja na mchango gani zaidi katika maboresho ya mkataba wa kimataifa ya udhibiti wa plastiki chini ya Umoja wa Mataifa programu ya Mazingira.

"Mawaziri wa nchi mbalimbali na viongozi walikaa mwaka 2022 na waliazimia mwaka 2024 kila nchi kuja na mkataba wa kimataifa ambao utakuwa ni mwongozo wa katika nchi mwanachama kufuata na kudhibiti uzalishwaji plastiki, ufangashaji, urejeleshi na mfumo mzima wa matumizi rejeshi."

Mratibu wa miradi kutoka Shirika Women Action Towards Economic Development in Tanzania, (WATED), Frida Chuwa, alisema lengo la mkutano huo ni kuwaita pamoja wadau kujadili na kuja na mawazo, maoni ya pamoja ili kuweka mikakati ya udhibiti wa taka hizo.

"Jamii bado hazina ufahamu mpana juu ya uhifadhi wa mazingira na kumekuwa na upatikanaji rahisi wa bidhaa za plastiki, pia sera na kanuni za plastiki hazitekelezeki kama ilivyo," alisema.





# Maandalizi maandamano ya CHADEMA Mbeya yaiva

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI mbalimbali wa kitaifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wanatarajiwa kushiriki maandamano ya amani yanayofanyika leo jijini Mbeya ikiwa ni mwendelezo wa ratiba ya maandamano ya chama hicho kwenye mkoa mbalimbali.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote maarufu China wa China, aliyasema hayo jana alipokuwa anatoa ratiba na ramani ya maandamano hayo.

Aliwataja viongozi wakuu wa chama hicho watakaoshiriki maandamano hayo kuwa ni Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa Chama, Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa Taifa, John Mnyika na wenyeviti wa kanda zote za chama hicho.

Alisema maandamano hayo yataanza asubuhi na kwamba kutakuwa na njia tatu ambazo wananchi wataandamana ambazo ni kuanzia Mbalizi ambako waandamanaji watatembea umbali wa zaidi ya kilomita 10, Uyole zaidi ya kilomita nane na njia ya Chunya ambayo waandamanaji watatembea kilomita nne.

Alisema viongozi hao wa kitaifa watagawana njia ambapo Mbowe na Katibu Mkuu wataanzia Mbalizi ambako wataambatana na wananchi wa kutoka katika mikoa ya Songwe na Rukwa, Makamu Mwenyekiti Lissu ataanzia njia ya Uyole ambako ataambatana na wananchi wa mikoa ya Iringa na Njombe.

Alisema maandamano hayo yataishia katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe ambapo viongozi wetu watahutubia na kuueleza umma kuhusu mambo mbalimbali ya kitaifa.

"Kuna watu wanapotosha kwamba maandamano haya ni ya CHADEMA, lakini iwaambie kwamba maandamano haya ni ya Watanzania wote na CHADEMA ni waratibu tu, tunaandamana ili kufikisha malalamiko yetu serikalini," alisema China.

Alisema walishapata kibali cha kuandamana kutoka Jeshi la Polisi na juzi walifanya kikao na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo kwa ajili ya kuelezea ramani itakayotumika kwenye maandamano hayo na kupokea miongozo mbalimbali. Hata hivyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga, alisema wao walishawajibu viongozi wa CHADEMA kuhusu maombi yao ya kutaka kufanya maandamano lakini hakusema kama walishatoa kibali.

Vilevile, alipoulizwa kuhusu kuimarisha ulinzi kwenye maandamano hayo, Kamanda Kuzaga alisema yupo kwenye kikao na kwamba jambo hilo lilikuwa ni miongoni mwa ajenda za kujadili.

"Sisi tulishawajibu CHADEMA kuhusu maombi yao, kwa sasa nipo kwenye kikao naomba mnitafute kuanzia saa nane mchana ili niwapatie majibu," alisema Kuzaga.

Maandamano ya CHADEMA yalianza jijini Dar es Salaam, Mwanza na kwa leo yanafanyikia jijini Mbeya ambako yataunganisha wanachama na wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyasa.



Kaimu Mkurugenzi wa Usajili Majina ya Biashara wa Kampuni ya Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA), Isdor Nkindi, akiwasilisha mada kwenye mafunzo kuhusu umiliki manufaa kwa baadhi ya wadau wa wakala huo jana jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## RPC Mbeya awataka polisi kutunza miti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMANDA wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, amewataka maaskari mkoani humo kutunza miti ambayo imepandwa katika maeneo yao ili kutunza mazingira.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akiongoza maofisa, wakaguzi na askari kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali ya kuzunguka uwanja wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoa wa Mbeya.

Kamanda Kuzaga alisema kuwa, upandaji wa miti katika maeneo ya kambi za polisi, vituo vya polisi na maeneo mengine ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Camillus Wambura la kutunza mazingira.

Aliongeza kuwa upandaji wa miti huo utafanyika katika wilaya zote sita za Kipolisi za Mkoa wa Mbeya ambapo kila askari amekabidhiwa mche wa mti kwa ajili ya kupanda na kuhakikisha anautunza ili kufikia malengo ya jeshi na nchi kwa ujumla.

"Tumeanza leo (juzi), jumla ya miche ya miti ya matunda na kivuli 1,000 aina ya Kassuarina, Pinuspatula, Misongwa na Mizambarao imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema IGP Wambura aliwataka makamanda wa mikoa kusimamia upandaji wa miti kwenye maeneo mbalimbali yanayozunguka vituo vya polisi na makazi ya askari kwa lengo la kutunza mazingira.

Mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliagiza wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kushirikiana na viongozi wa Kamati ya Amani na maridhiano kupanda miti kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya kutunza mazingira.

Homera alitoa agizo hilo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ratiba ya maadhimisho ya Wiki ya Amani na Maridhiano ambayo inatarajiwa kufikia kilele Machi 6, mwaka huu na kitaifa yanatarajiwa kufanyika jijini Mbeya.

# RC awaonya madereva magari serikali kusafirisha dawa kulevya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, ameonya tabia ya baadhi ya madereva wa magari ya serikali kuyatumia magari hayo kubeba dawa za kulevya ikiwamo bangi, kupiga ving'ora bila sababu pamoja na kuendesha magari wakiwa wamelewa.

Mtaka aliyasema hayo wakati wa kukabidhi magari 13 ya kubeba wagonjwa na ya idara ya afya kwenye halmashauri sita za mkoa huo pamoja na Chuo cha Uuguzi cha Kibena makabidhiano ambayo yalifanyika kwenye ofisi za mkoa huo.

"Nakabidhi magari haya kwa ajili ya kwenda kutoa huduma kwa wananchi wa mkoa wa Njombe, hivyo yatumieni magari haya kwa malengo kusudiwa ili wananchi wapate huduma bora za matibabu," alisema Mtaka.

"Kwenye wilaya ambazo tumekabidhi magari hebu nendeni na haya magari mkafanye uzinduzi hadi kwa wananchi ili madiwani wajue wanapojadili wajadili uhalisia wa maisha ya watu," alisema Mtaka.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, alisema magari hayo yakasaidie kwenda kutoa huduma za afya katika vituo vyote 340 na kuongeza chachu ya ufuatiliaji.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. David Ntahindwa, alisema kuwa magari hayo yatasaidia kuongeza usimamizi katika vituo vya afya na kusafirisha wagonjwa wa dharura.

"Mkoa wetu umepata jumla ya magari 13 ambapo magari saba ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa na magari matano ni kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya na gari moja ilikuwa ni kwa ajili ya chuo cha wauguzi na wakunga Kibena na hospitali ya rufani imepata magari mawili," alisema Ntahindwa.

Dk. Ntahindwa alisema magari hayo yatasaidia kuongeza usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, aliwataka madereva kuhakikisha wanazingatia taratibu za kuendesha magari ili yaweze kudumu na dhamira ya kuokoa wananchi iweze kutimia.

"Tumekuwa tukishuhudia gari imekabidhiwa kwa mfano Dodoma au Dar Es Salaam halijafika kwenye kituo kinachotakiwa kufika limeshapata ajali na ukiangalia kutoka huko kulikuwa na uzembe wa dereva wa kutokuzingatia sheria.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Dk. Frank Mganga, alikiri kuwapo kwa changamoto kubwa ya usafiri katika vituo vya kutolea huduma za afya.

"Ni kweli kinamama walikuwa wakijifungua katika hali ngumu sana kuna baadhi ya maeneo kinamama wajawazito wanasafiri hadi km tatu na namna ya kupanda pikipiki anatakiwa amlalie dereva ili pikipiki isirudi nyuma," alisema Mganga.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi mkoani Njombe akiwamo Francis Nindi na Christina Mzena mbali na kushukuru kwa kuletwa kwa magari hayo lakini wanaomba yawe msaada pindi wanapokumbwa na changamoto za kiafya huko uraiani.



## Wanaofanya uvuvi haramu waonywa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu imesema haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya wavuvi wanaofanya shughuli haramu katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria ya Uvuvi namba 10 ya mwaka 2010.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Shaaban Ali Othman katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akitoa ufafanuzi wa matumizi ya sheria ya uvuvi ya mwaka 2010 inayopiga marufuku matumizi ya uvuvi katika maeneo ya hifadhi yaliopo Unguja na Pemba.

Alisema serikali imetenga jumla ya maeneo 11 chini ya hifadhi ya bahari ya uvuvi ambapo lengo lake ni kuongeza tija ya uzalishaji wa bidhaa ya samaki na kuwawezesha wavuvi kupata kipato zaidi.

Aidha, alisema lengo la sheria ya uvuvi katika maeneo ya hifadhi kuhakikisha kwamba viumbe vya bahari ikiwemo samaki na matumbawe wanalindwa na athari za uharibifu unaofanywa na wavuvi wasiokuwa waaminifu.

Alisema hatua hizo zilichukuliwa baada ya kubainika kwamba baadhi ya samaki walikuwa katika tishio la kutoweka duniani kutokana na uvuvi haramu uliokuwa ukifanywa ikiwemo Pweza, Ngisi pamoja na Kamba.

"Wizara ya uvuvi na uchumi wa buluu tutahakikisha kwamba maeneo ya hifadhi yanalindwa ili kuepuka uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi wasiokuwa waaminifu ambao hufanya uharibifu katika mazalia ya samaki ikiwemo matumbawe,"alisema.

Waziri Shaaban alisema maeneo ya hifadhi hayatakiwi kutumiwa mitego hatari tishio kwa maisha ya viumbe vya baharini ikiwemo nyavu zenye macho madogo.

Aidha, aliitaja mitego mengine ikiwemo kutumiya "umangu" ambao huharibu na kubomowa matumbawe ambayo ndiyo mazalia ya samaki.

"Wizara ya uvuvi na uchumi wa buluu tutahakikisha sheria ua uvuvi ya mwaka 2010 inafanya kazi zake katika kudhibiti matukio ya uvuvi haramu unaotishia maisha ya viumbe vya baharini na matumbawe,"alisema.

**Waziri Shaaban alisema maeneo ya hifadhi hayatakiwi kutumiwa mitego hatari tishio kwa maisha ya viumbe vya baharini ikiwemo nyavu zenye macho madogo.**

# Biashara haramu viumbepori ilivyotishio kwa uchumi, jamii

**Na Rahma Suleiman,** aliyekuwa Bagamoyo

BIASHARA haramu ya viumbe pori ni tatizo la kimataifa na haliathiri Tanzania pekee bali duniani kutokana na athari zake kiuchumi na kijamii. Imeelezwa na Mkuu wa Kitengo cha Sera na Usimamizi wa Maliasili USAID Tuhifadhi Maliasili, Allan Mgaza.

Aliyasema hayo wakati akiwasilisha mada ya biashara haramu ya wanyamapori kwa waandishi wa habari katika mafunzo ya uhifadhi wa maliasili yaliondaliwa na jumuiya ya waandishi wa habari za mazingira Tanzania (JET) chini ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili yaliofanyika Wilayani Magamoyo.

Mkuu huyo alisema biashara haramu ya viumbe pori inachukua nafasi ya nne kati ya biashara haramu kimataifa, ambapo biashara hiyo hufanyika kwa usiri mkubwa na wafanyaji wa biashara hizo huwa na mawasiliano ya siri na husafirisha mizigo bila ya wasimamizi wa sheria kuwaona.

Alisema wanahabari wanajukumu kubwa la kutoa elimu kwa jamii kwa sababu jamii inahusishwa katika biashara hiyo aidha kwa kujua au kwa kutojua na bila ya kujua madhara kwa taifa na namna madhara yanavyomuathiri mtu mmoja mmoja. "Waandishi wa habari ni vyema wakatoa elimu katika kupambana na biashara hii haramu ya viumbe pori na lazima kushirkiana kuungana pamoja katika kupambana na biashara hii,"alisema.

Aidha, alisema kufanya biashara hiyo ni kuliangusha taifa kwasababu taifa linakosa kipato na kupoteza viumbe na mwisho wa siku viumbe hivyo kupotea na vizazi vijavyo kutofaidika na viumbe hivyo.

"Viumbe vinavyofanyiwa biashara haramu ni vingi ikiwemo mimea ya misitu kama Msandali, lakini pia Mnyama wa Kaka kuona ambae anaanza kutoweka, Tembo na Kima, biashara hiyo ikiendelea kufanyika kutakuwa hakuna wanyamapori,"alisema Mgaza.

Hata hivyo, alisema Tanzania imesaini mkataba wa kimataifa unaodhibiti biashara ya kimataifa ya viumbe pori ambavyo vipo hatarini kutoweka na nchi inasheria nzuri ya kudhibiti biashara hivyo ni vyema kueendelea kutoa uelewa wa usimamizi wa sheria hizo.

Doresin Nyoni, Afisa ufatiliaji na tathmini katika mradi wa USDAID Tuhifadhi Maliasili, alisema mradi huo wa USAID Tuhifadhi maliasi unamalengo ya kuwajengea uwezo wanawake ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za uhifadhi.

Alisema kupitia kampeni mbalimbali shuleni huwafundisha watoto jinsi ya kuhifadhi maliasili na kutoa elimu ya uhifadhi inayotolewa katika shoroba na kuna mabadiliko makubwa, ikiwemo kushiriki katika operesheni za maeneo ya hifadhi yanayolindwa, kufanya shughuli rafiki kwenye uhifadhi na kujua mbinu sahihi ya kuboresha vikundi vyao.

Aidha, alisema mchango wa wanawake katika uhifadhi ni mkubwa ingawa zipo baadhi ya changamoto zinazowakabili wanawake ikiwemo kuhusihwa katika biashara haramu ya wanyamapori aidha kwa kujua au kutojua.

Mwenyekiti ya JET, Dk. Hellen Otaru, alisema wanawake lazima washirikishwe katika utunzaji wa ardhi na mazingira na asipopata elimu ataendelea kuharibu na kukataza vyanzo vilivyomo katika ardhi haitosaidia lazima kueleweshwa badala ya kutotumia kuni au mkaa mbadala wake ni upi.

Alisema wanawake wanahitaji kushirkishwa jinsi ya kujipatia mahitaji yao muhimu na kujikimu kiuchumi kwa kutomia vyanzo asili ambavyo vinaharibika.

Aidha alisema kutokana na kupotea kwa viumbe, wadudu na wanyamapori kutokana na athari za kimazingira ikiwemo mabadiliko ya tabianchi ni vyema waandishi wa habari kufanya uchechemuzi na kuelimisha jamii juu ya mabadiliko ya sera ili kukabiliana na athari hizo.



Wafanyabiashara ndogondogo maarufu 'Wamachinga' wakiwa wamepanga biashara zao kwenye miundombinu ya barabara, eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam juzi. Uhaba wa wateja kwenye masoko umekuwa ni changamoto kwao, ambayo inasababisha 'wavamie' hata maeneo yasiyo rasmi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Baraza lataka serikali kukarabati majengo chakavu ya magereza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetakiwa kuyafanyia ukarabati majengo ya Magereza ambayo baadhi yake hayana ubora wa kutoa huduma kwa wafungwa.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mariyam Thani Juma wakati akiwasilisha taarifa ya ripoti ya kamati ya viongozi wakuu wa kitaifa mbele ya baraza la wawakilishi huko Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar.

Mwenyekiti huyo aliyataja Magereza ya Wete Pemba pamoja na makao makuu Kilimani Unguja kwamba yanahitaji ukarabati mkubwa, ili kwenda na wakati na kutoa huduma kwa wafungwa zinazokwenda na mabadiliko ya wakati uliopo sasa.

Kwa mujibu wa Mariyam, Gereza la Wete linahitaji ukarabati wa jengo lake kwa ajili ya kutoa huduma bora za wafungwa ambazo zinakidhi mahitaji ya haki za binaadamu.

"Mheshimiwa Spika gereza la Wete linahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa ili kwenda na wakati uliopo sasa wa mahitaji yake katika kutoa huduma kwa wafungwa zinazokwenda katika dhana ya utawala bora,"alisema.

Aidha, alisema kamati imesikitishwa na mlundikano mkubwa wa mahabusu uliopo katika gereza kuu la Kiinuwa miguu Kilimani Unguja.

Alisema kamati ya viongozi wakuu wa kitaifa inashauri Chuo cha Mafunzo kulihamisha gereza hilo kutoka Kilimani na kulipeleka Hanyegwamchana nje ya mji wa Zanzibar eneo lenye nafasi kubwa kwa wafungwa kufanya shughuli mbalimbali.

Baadhi ya wawakilishi waliochangia ripoti hiyo wameitaka serikali kuharakisha kesi zinazowahusu watuhumiwa na kuona zinatolewa hukumu yake kwa sababu wapo wengine wamekaa muda mrefu bila ya kushtakiwa ikiwemo wanaotuhumiwa na makosa ya mauaji.

Mwakilishi wa jimbo la Kojani, Hassan Hamad Omar alisema wapo watuhumiwa wanachukuwa muda mrefu hadi kesi zao kutajwa mahakamani kitendo ambacho kinakwenda kinyume na haki za binaadamu na utawala bora.

Alisema hatua hiyo inatakiwa kwenda sambamba na kukamilisha uchunguzi wa mashauri mbalimbali ikiwemo kesi zinazowakabili watuhumiwa kutoka kwa jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka (DPP).

## Israel yatishia kuishambulia Rafah wakati wa Ramadhan

**TEL AVIV,** ISRAEL

ISRAEL imetishia kuvamia mji wa Rafah ndani ya Ukanda wa Gaza ifikapo mwanzo wa mwezi mtukufu kwa Waislamu wa mfungo wa Ramadhan, endapo mateka wanaoshikwa na wanamgambo wa Hamas hawatakuwa wameachiliwa huru.

Inaelezwa kuwa kauli hiyo imetolewa huku Mahakama ya Haki ya Umoja wa Mataifa (ICJ) ikianza kusikiliza kesi ya kihistoria dhidi ya Israel kuhusu uhalali wake wa kuikalia ardhi ya Palestina kimabavu.

Huku matarajio ya mazungumzo ya mapatano yakiwa yamefifia, Marekani na Umoja wa Mataifa (UN), zimetoa wito wa dharura kwa Israel kusitisha mashambulizi yake yaliyopangwa dhidi ya Rafah.

Kwa mujibu wa serikali ya Israel, mji wa Rafah ulioko katika mpaka wa Gaza na Misri, ndio ngome ya mwisho iliyosalia ya wanamgambo wa Hamas.

Onyo la Israel limejiri licha ya shinikizo la kimataifa kutaka raia wengi wa Gaza waliokimbilia mji huo wa kusini mwa Gaza Rafah, walindwe.

Inakadiriwa kuwa robo tatu ya watu wote waliohamishwa na vita Gaza, walikimbilia Rafah, wakiishi kwenye mahema bila huduma za msingi za kutosha ikiwamo chakula, dawa na maji.

Benny Ganz, waziri katika Baraza la Mawaziri wa Vita la Israel alisema wanamgambo wa Hamas wanaweza kuchagua kati ya kujisalimisha au kuwaachilia huru mateka ili raia wa Gaza wafunge Ramadhan kwa amani.

"Ikiwa wanaoshikiliwa mateka hawatakuwa wameachiliwa huru ifikapo Ramadhani, mapigano yataendelea kote ikiwamo eneo la Rafah. Tutafanya hivyo taratibu, kuwezesha kuhamishwa kwa raia kuondoka, kwa mazungumzo na washirika wetu wakiwamo Marekani na Misri na kupunguza vifo vya raia kadri iwezekanavyo," alisema Ganz. **DW**

# Afrika yatajwa kukua kiuchumi

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imesema Afrika inaongoza katika orodha ya mataifa 20 yenye uchumi unaokua kwa kasi zaidi duniani mwaka huu, kwamba itachangia kwa kuwa katika nafasi ya 11 kati ya 20 za mataifa yanayaokua kwa kasi zaidi duniani.

Kwa mujibu wa ripoti ya uchumi mkuu, iliyotolewa na benki hiyo yenye makao yake makuu Abidjan, Ivory Cost, kwa ujumla ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa Bara la Afrika unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.8 na 4.2 mwaka 2024 na 2025. Na kwamba makadirio hayo ni ya juu kuliko wastani wa makadirio ya kimataifa ya asilimia 2.9 na 3.2.

Ilielezwa kuwa Bara la Afrika linatazamiwa kusalia kuwa eneo la pili kwa kukua kwa kasi baada ya Asia. Huku zikibainishwa nchi 11 bora Afrika zinazotarajiwa kuwa na ufanisi wa kiuchumi na asilimia katika mabano, ikiwamo Niger asilimia (11.2), Senegal (8.2), Libya (7.9), Rwanda (7.2), Cote d'Ivoire (6.8), Ethiopia (6.7). Benin (6.4), Djibouti (6.2), Tanzania (6.1), Togo na Uganda zikiwa na asilimia sita.

"Pamoja na changamoto ya mazingira ya kiuchumi ya kimataifa na kikanda, nchi 15 za Afrika zimeongeza upanuzi wa pato la zaidi ya asilimia tano," Rais wa Kundi la Benki hiyo Dk. Akinwumi Adesina alisema, akitoa wito wa kuwepo kwa fedha nyingi na uingiliaji kati wa sera ili kukuza zaidi ukuaji wa Afrika.

Ripoti ya hivi karibuni inatoa wito wa kuwa na tahadhari kutokana na changamoto za kimataifa na kikanda ikiwamo kuongezeka kwa mvutano wa kisiasa wa kijiografia, migogoro ya kikanda na ukosefu wa utulivu wa kisiasa na kwamba yote hayo yanaweza kuvuruga mtiririko wa biashara, uwekezaji na kuendeleza shinikizo la mfumuko wa bei.

Rais Adesina alieleza kuwa nakisi ya fedha imeimarika, kwa kuwa ahueni ya haraka kuliko ilivyotarajiwa kutoka kwenye janga hilo ilisaidia kuongeza mapato.

Alifafanua akieleza kuwa "Hii imesababisha utulivu wa wastani ya fedha kwa asilimia 4.9 mwaka 2023, kama mwaka 2022, lakini kwa kiasi kikubwa chini ya wastani wa 6.9 ya 2020. Utulivu huo pia unatokana na hatua za ujumuishaji wa fedha, haswa katika nchi zilizo na hatari kubwa ya dhiki ya madeni."

Pia alitahadharisha kuwa kutokana na hali ya uchumi wa dunia kutokuwa na uhakika, nafasi za kifedha za bara la Afrika zitaendelea kukabiliwa na misukosuko ya kimataifa.



Mahakama ya Haki ya Umoja wa Mataifa (ICJ) ikisikiliza kesi dhidi ya Israel kuhusu uhalali wake wa kudhibiti ardhi ya Wapalestina. **PICHA MTANDAO.**

# Mawazo mseto yaibuka kuhusu mrithi wa Museveni Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

MATAMISHI ya Waziri wa Mambo ya Ndani wa Uganda, Jenerali Kahinda Otafire, ambaye ameonya kuwa Waganda watajilaumu wenyewe ikiwa wataruhusu kiongozi wa kiimla kumrithi Rais Yoweri Museveni yamepokelewa na maoni mchanganyiko.

Kwa mujibu wa baadhi ya wanasiasa na wadadisi, jenerali huyo anafichua kuhusu mkakati wa kumrithisha mwanawe Rais Museveni, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, na kwamba wampongeza kwa kudhihirisha kuwa hata yeye hafurahii hali hiyo.

Akiwa kwenye kumbukumbu za mauaji ya aliyekuwa Askofu Mkuu wa Kanisa la Kianglikana, Janan Luwum, juzi, waziri huyo alinukuliwa na vyombo vya habari akisema "tahadharini kuhusu wale wanaowahadaa kwamba sisi ndiyo tutakuwa suluhu kwa shida zenu, wanajitakia makuu na nisingependa kuitumbikiza nchi hii katika hali mbaya ya utawala wa kiimla."

Matamshi hayo yametafsiriwa kuwa yanalenga kuwaonya Waganda kuhusu hila na mkakati wa utawala kumtegenezea njia mwanawe Rais Museveni, Jenerali Muhoozi, kumrithi baba ake.

Kwa mujibu wa mdadisi wa mambo ya kisiasa John Kibego, onyo na tahadhari za jenerali huyo zinatakiwa kutiliwa maanani kwani ni ishara kuwa kuna hila za utawala wa sasa kupokeza kwa kiongozi ambaye hatakuwa mwenye tija kwa taifa hilo la Afrika Mashariki.

"Jenerali Otafire ametufichulia hali ilivyo na sasa tunatakiwa kuchukua tahadhari kuhusiana na viongozi wanaotaka kutwaa madaraka," alisema mchambuzi huyo wa masuala ya kisiasa.

Baadhi ya wafuatiliaji wa siasa za Uganda wamekosoa hadharani na matamshi ya kiongozi huyo, kuwa nae ni sehemu ya utawala huo uliokaa madarakani kwa zaidi ya miaka 38.

Mmoja wa wanasiasa hao akiwamo Asha Nantongo, alieleza kuwa kiongozi huyo naye anawajibika katika mapungufu ya utawala wa kuwaweka raia hasa vijana katika mashaka kuhusu mustakabali wao.

"Umekuwa sehemu ya utawala ambao umewatumbukiza watu katika hali ya mashaka na umaskini na kwa hiyo hata wewe unawajibikia kwa makosa ya utawala," alisema Nantongo. **DW**

# KIDUNDA, MBABE WA KIDUKU KUWANIA MKANDA WA WBF

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Selemani Kidunda, anatarajia kupanda ulingoni Machi Mosi, mwaka huu, katika pambano la raundi 12 la kuwania mkanda wa WBF dhidi ya mpinzani wake, Asemahle Wellem kutoka Afrika Kusini.

Katika pambano hilo linalotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam, Wellem atakuwa akitetea mkanda huo alioupata mwaka jana baada ya kumpiga Twaha Kiduku.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Fayheroes, Abdul Salim, alisema maandalizi yameenda vizuri kuhusu pambano hilo ambalo litakuwa la raundi 12 huku likisindikizwa na mabondia zaidi ya 20.

Alisema mbali na Kidunda dhidi ya Wallem ambalo ndilo pambano kubwa siku hiyo, pia kutakuwa na mapambano kusapoti kati ya Ramadhani Nassib na Emmanuel Nadjala kutoka Malawi.

"Mabondia wote kutoka nje ya Tanzania ambao tumeingia nao mkataba na watakaopanda ulingoni, wanatarajiwa kutua nchini Februari 27, mwaka huu. Tumefanya uwiano mzuri kwa mabondia ambapo asilimia 50 ni kutoka hapa nyumbani na 50 kutoka mataifa mengine," alisema Abdul.

Alisema siku hiyo kutakuwa na mapambano 10 ya utangulizi ambapo Hamad Furahisha atapanda ulingoni dhidi ya Ally Mwerange, wakati Lupakisyo Shoti atapigana na Jacob Maganga wote kutoka Tanzania.

„Salim Jengo (Tanzania), atacheza dhidi ya Gray Chimkwapulo (Malawi), Mohammed Hamad (Tanzania) atazichapa na Aidin Muzei (Uganda), Omary Sultan dhidi ya Salim Athuman na Loren Japhet atapanda ulingoni kuzichapa na Hillary Katuya (Zambia)," alisema.



Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, akizungumzia uzinduzi wa 'Mtoko wa Kibingwa' utakaowapa mashabiki 56 fursa ya kushuhudia dabi ya Simba na Yanga itakayopigwa Aprili mwaka huu. Kushoto kwake ni Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Alec Wehbe. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashabiki 56 'Mtoko Kibingwa' kushuhudia dabi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI watani wa jadi, Simba na Yanga wakitarajiwa kushuka uwanjani Aprili kwenye mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, mashabiki 56 wa ‚Betika Mtoko wa Kibingwa' wamepewa nafasi kuishuhudia bure.

Mashabiki hao ambao ni washindi wa msimu wa saba wa droo ya Mtoko wa Kibingwa wataishuhudia dabi hiyo kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Betika.

Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, katika uzinduzi wa droo hiyo jana alisema kila wiki kutakuwa na washindi wanane watakaopata fursa hiyo.

„Lengo ni kuwapa fursa mashabiki wa Simba na Yanga kuishuhudia dabi hiyo mubashara kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Betika," alisema.

Alifafanua kwamba ili kupata fursa hiyo ni kusuka mkeka wako kuanzia mechi tatu na kuendelea kwa kuweka dau la kuanzia Sh. 2,000.

„Mbali na kuingia kwenye droo ya kuishuhudia dabi mubashara, pia kila wiki tutakuwa na washindi wawili wa simu janja na kila mwezi tutakuwa na mshindi mmoja wa Iphone 15," alisema Rugambwa.

Alisema washiriki wote wataingia kwenye droo kubwa ya kutafuta nafasi ya kuishuhudia dabi hiyo ya watani wa jadi mubashara.

„Kama kawaida yetu Betika, washindi wote watalala kwenye hoteli ya nyota tano, watakwenda kwa king'ora uwanjani na kukaa VIP. Droo yetu inafanyika kote nchini, wale washindi kutoka mikoani tutawalipia usafiri wa ndege kuja na kurudi," alisema.

Akizungumzia droo hiyo, Rugambwa alisema imeweza kuwaleta mashabiki 350 kushuhudia dabi hiyo tangu ilipoanza.

Alisema droo ya kwanza itakuwa Februari 27, mwaka huu ambayo itatoa washindi wanane na itafanyika kwa wiki saba.

„Bila kujali kama mkeka utachanika au la, kila atakayebashiri nasi ataingia kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa yenye kauli mbiu ya ‚Kaa kwa Kutulia'," alisema.

## Zimamoto: Bado tuna nafasi ya ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa Zimamoto SC, wamesema licha ya kusuasua kupata matokeo mazuri katika michezo miwili ya mzunguko huu wa lala salama hawatojiondoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Zimamoto imepoteza michezo miwli mfululizo katika mzunguko huu wa lala salama katika michezo mitatu waliyocheza.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Hilali, alisema bado wataendelea kuwa miongoni mwa timu zinazopigania taji la Ligi Kuu Zanzibar bila kuangalia michezo waliyopoteza.

Alisema ni mapema mno kukata tamaa katika mbio hizo kwa kuwa bado wana michezo 12 katika mzunguko huu hivyo ana matumaini makubwa katika michezo hiyo iliyosalia wataweza kusawazisha makosa yao na kupata matokeo mazuri.

Hilali alisema anaendelea kuwajenga wachezaji wake kisaikolojia hasa katika harakati hizi za ubingwa ili kutotoka mchezoni na kuendelea kupambana hadi kutimiza lengo lao.

"Bado ligi ni ngumu sana na ugumu huu ndio unatupa matumaini ya kuhakikisha tunafanikiwa lengo letu hasa katika mbio mbio za ubingwa, hatukufanya vizuri michezo miwili ya mzunguko huu, hii imetupa mwanga kuwa mzunguko huu tuendelee nao vipi," alisema.

Aidha, alisema kuelekea mchezo wao wa 19 dhidi ya vinara wa ligi hiyo, JKU SC, wamejipanga kuhakikisha wanapata alama tatu ambazo ni muhimu katika safari yao.

Alisema anajua utakuwa mchezo mgumu na wenye uhitaji wa alama tatu kwa kila upande, hivyo atatumia mbinu ambayo itamchanganya mpinzani wake ili kushinda mechi hiyo.

"Mchezo huu unahitaji kutumia mbinu ambazo zinatafanikisha kupata alama tatu, kwa kuwa mpinzani wetu na yeye hakupata matokeo mazuri kwa mechi mbili mfululizo na ikizingatiwa sote tupo katika lengo la ubingwa, hivyo lazima kila mmoja atakuja na mbinu ya kuhakikisha hapotezi mchezo," alisema.

Zimamoto SC ipo nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 33, wakati nafasi ya kwanza inashikiliwa na JKU SC wenye alama 40, ikifuatiwa na bingwa mtetezi, KMKM wenye alama 38 na nafasi ya tatu inashikiliwa na Maafande wa KVZ wenye alama 33.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATETA NA CITY

KYLIAN Mbappe alifanya mazungumzo na Manchester City siku moja kabla ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25, kutangaza kuwa anaondoka Paris St-Germain mwishoni mwa msimu. **(Cadena Ser)**

### ASHWORTH ANUKIA UNITED

MKURUGENZI wa Michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth, amewekwa kwenye likizo baada ya kuomba kuondoka klabuni hapo huku Manchester United ikiwa na nia ya kumsajili. **(Mail)**

### KANE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inafuatilia hali ya Harry Kane katika Klabu ya Bayern Munich huku kukiwa na ripoti kwamba mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 30, hana furaha kabisa nchini Ujerumani. **(Football Insider)**

### LIVERPOOL NA ALONSO

LIVERPOOL wana matumaini kumnasa Kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso na Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Simon Rolfes, kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp na Jorg Schmadtke wanaoondoka msimu huu. **(Football Insider)**

### GARNER AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumnunua kiungo wa kati wa Everton, James Garner, 22, msimu wa joto. **(TeamTalks)**

### GLASNER KUMRITHI HODGSON

OLIVER Glasner amekubali mkataba wa miaka miwili na nusu kumrithi Roy Hodgson kama kocha wa Crystal Palace. **(Sky Sports)**

### GLOUKH ACHUNGUZWA

KLABU ya Arsenal ilimchunguza kiungo wa kati wa Red Bull Salzburg, Oscar Gloukh, Jumamosi wakati wanafikiria mbinu ya kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Israel mwenye umri wa miaka 19. **(Football Transfers)**

### COLEMAN KUIBUKIA IRELAND

KOCHA wa zamani wa Wales, Chris Coleman, ameibuka kuwania nafasi ya kuinoa Jamhuri ya Ireland baada ya mazungumzo na kocha wa timu ya vijana ya chini ya miaka 21, Lee Carsley kukwama. **(Independent)**

### TUCHEL HATIMULIWI BAYERN

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, hatatimuliwa licha ya timu hiyo ya Bundesliga kupata kipigo cha tatu ndani ya siku tisa dhidi ya Bochum Jumapili. **(Sky Germany)**

### ZEBRIN NA BARCELONA

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, ameomba ripoti zaidi za uchunguzi kuhusu Roberto de Zerbi anapofikiria kumkaribia bosi wa Brighton ili kumrithi Xavi kama kocha mwishoni mwa msimu huu. **(Sport)**

### LONG HUYOOO MSL

MLINZI wa Birmingham na Jamhuri ya Ireland, Kevin Long mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kukamilisha uhamisho wa kwenda Toronto FC ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS. **(Birmingham mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: SARE YETU SABABU SI MBAPPE

Wakati mambo hayakwenda vizuri, kukosoa timu hii msimu huu ni ngumu, kwani...

**VALLECAS, Hispania**

CARLO Ancelotti amesisitiza kwamba wachezaji wa Real Madrid hawajatingishwa na mazungumzo yanayohusisha klabu hiyo na Kylian Mbappe baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Rayo Vallecano Jumapili na kuacha wazi mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Joselu aliwaweka wageni mbele dakika ya tatu huko Vallecas, kabla ya fowadi wa zamani wa Madrid, Raul de Tomas kusawazisha kwa mkwaju wa penalti na beki Dani Carvajal kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika muda wa nyongeza. Matokeo hayo yanaiacha Madrid - ambayo nafasi yao ya kutua kwa Mbappe iliongezeka wiki hii, baada ya fowadi huyo kuifahamisha Paris Saint-Germain kwamba anatarajia kuondoka msimu huu wa majira ya joto - pointi sita juu ya jedwali la LaLiga, kabla ya Girona inayoshika nafasi ya pili kucheza jana Jumatatu dhidi ya Athletic Club.

„Ni wakati gani hatujazingatia?" Alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, alipoulizwa kama vichwa vya habari vinavyomzunguka Mbappe vilikuwa ni usumbufu kwa wachezaji.

„Nadhani tumekuwa tukizingatia. Na leo (juzi) pia, wakati mambo hayakwenda vizuri. Kukosoa timu hii msimu huu ni ngumu."

„Tulianza vizuri sana na kufunga mapema," aliongeza Ancelotti. „Baada ya penalti ya Rayo, mchezo ulibadilika, kulikuwa na mpambano zaidi, ilikuwa vita zaidi. Ni sare ambayo hatufurahii, lakini tutaendelea. Tuko vizuri.

„Lazima tushinde kila mchezo, lakini ili kushinda ligi ni muhimu ikiwa huwezi kushinda usipoteze. Wakati mwingine sare inaumiza, lakini mwisho inaweza kuwa hatua nzuri ya kutusaidia kushinda ligi."

# TUCHEL AAPA KUBADILISHA MAMBO BAYERN MUNICH

**MUNICH, Ujerumani**

THOMAS Tuchel amesisitiza kuwa anaweza kurekebisha mambo yote ndani ya Bayern Munich licha ya kuona timu yake ikipoteza mchezo wao wa tatu mfululizo wa mashindano kwa mara ya kwanza tangu Mei mwaka 2015, juzi Jumapili.


Bayern walichapwa 3-2 na VfL Bochum na kuongeza shinikizo kwa kocha huyo wa Mjerumani, ambaye tayari alikuwa alipokea kipigo cha mabao 3-0 wikendi iliyopita kutoka kwa kikosi cha Xabi Alonso, Bayer Leverkusen.

Bayern sasa wapo pointi nane nyuma ya Leverkusen ambayo haijapoteza baada ya michezo 22 ya kampeni ya Bundesliga.

"Ukiniuliza, ikiwa bado ninaamini kwa dhati naweza kubadilisha mambo - jibu ni ndio," alisema Tuchel baada ya kufungwa na Bochum.

"Kuongezeka kwa shinikizo? Hiyo hutokea baada ya kila unapopoteza. Lakini leo (juzi) hatujaacha, hatukuacha kujaribu."

Tuchel anaweza kufarijiwa na maoni yaliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Bayern, Jan-Christian Dreesen baada ya mchezo huo alipoulizwa ikiwa mshindi huyo wa Ligi ya Mabingwa wa mwaka 2021 ataendelea kuwa kocha katika mchezo ujao wa timu hiyo dhidi ya RB Leipzig.



"Bila shaka," alisema Dreesen. „Mimi si shabiki wa taarifa mbaya.

"Lakini hili la mustakabali wa Tuchel si suala ambalo tunashughulikia kwa sasa. Tunapaswa kuzingatia mechi zetu zijazo."

Kiungo wa kati wa Bayern, Leon Goretzka, alilinganisha mwendo wa Bayern wa kupoteza - na Leverkusen, Lazio katika Ligi ya Mabingwa na sasa Bochum na filamu ya kutisha.

"Inahisi kama sinema ya kutisha ambayo haimaliziki. Kila kitu kinakwenda kinyume na sisi kwa sasa," alisema.

"Tunaweza tena kukaa hapa na kusema tumeanza vizuri. Lakini sasa unajiona mjinga kujiwekea kikomo kwa nusu saa. Mwishowe tulijaribu kila kitu, kwa hivyo huwezi kutulaumu."

## Ten Hag akunwa na uwezo wa Hojlund

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alisifu tabia ya Rasmus Hojlund baada ya Mdenmark huyo kufunga mara mbili katika dakika saba za kwanza na kuisaidia Manchester United kuishinda Luton mabao 2-1.

Baada ya kuanza polepole katika uchezaji wake pale Old Trafford, mshambuliaji huyo - aliyesajiliwa kutoka Atalanta kwa pauni milioni 72 - sasa amefunga katika mechi sita mfululizo na kumfanya kuwa na mabao 13 katika mechi 30 za kwanza za United.

Huku United wakipanua mbio zao za ushindi kwenye ligi hadi mechi nne ili kuweka shinikizo kwa Aston Villa na Tottenham Hotspur katika mbio za nne bora, Ten Hag aliamua kumsifia Hojlund mwenye umri wa miaka 21.

Ten Hag alisema: „Tunafurahi sana, kwamba tulisajili mchezaji anayefaa kwa sababu anaweza kufanya kazi chini ya mkazo.

"Na mambo yanapomwendea kinyume kama kipindi cha kwanza cha msimu, ana uwezo wa kuwa na tabia dhabiti, mvumilivu, kuamua na kufunga mabao na ndivyo tulivyoona tulipomchunguza.

„Kwa kweli, alihitaji msaada kwa sababu si rahisi sana ukiwa mdogo, lakini kwa ujumla, alitulia na unaona uwezo wake."

Ilimchukua Hojlund hadi Boxing Day kufunga bao lake la kwanza la ligi akiwa na United, akifunga bao la ushindi dakika za lala salama katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Villa Uwanja wa Old Trafford.

Ten Hag aliongeza: „Mwanzoni hakuwa na bahati sana. Alifunga baadhi ya mabao, kwa mfano, lile dhidi ya Brighton, mechi yake ya kwanza, na walikataa na hakuna anayejua ni kwa nini.

„Kuna nyakati ambazo ni muhimu sana katika klabu mpya na ligi mpya, hasa kwa mshambuliaji kujenga kujiamini.

"Hiyo hakupewa lakini unaona ni mpambanaji, anaendelea na ana uwezo mkubwa mbele ya goli. Lakini tulichoona tangu Septemba ni kwamba anaimarika katika maeneo mengine mengi kama vile kushikilia mpira."




## PSG yajiandaa kumtwaa Osimhen

**PARIS, Ufaransa**

IMEFAHAMIKA kuwa mabosi wa Paris-Saint Germain wanahaha kutafuta mbadala wa Kylian Mbappe ambaye ameshawataarifu kwamba ataondoka mwishoni mwa msimu huu kama mchezaji huru.

Kwa sasa mabosi hao wanafikiria kumshusha nyota wa Kimataifa wa Nigeria na Napoli ya Italia, Victor Osimhen, na wanaona nyota huyo ambaye mkataba wake na mabingwa hao wa Serie A utamalizika mwaka 2026, atawafaa zaidi.

Awali, PSG ilikuwa ikipambana kuona itafanya nini ili Mbappe asiondoke bure na angeongeza mkataba mpya utakaoipa faida kutokana na mauzo yake.

Hata hivyo, kwa sasa haitanufaika naye kwani anaondoka bure.

Osimhen mwenye umri wa miaka 25, alionyesha kiwango bora msimu uliopita akiwa na Napoli na kuipa ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia na akiibuka pia mfungaji bora wa ligi.

Hata hivyo, inaonekana ni vigumu kumpata kwa urahisi kwa kuwa Napoli inahitaji zaidi ya euro milioni 100 na kuna utitiri wa timu nyingi zinazopambana kumsajili.



# MANULA AWAPA SOMO WAZAZI KUHUSU VIPAJI

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI wametakiwa kuwapa ushirikiano watoto wao katika kukuza na kuendeleza vipaji vyao ili kutimiza ndoto zao pale wanapoonyesha uwezo kwenye mchezo wowote, jambo ambalo litasaidia kuwapata kina Mbwana Samatta, John Boko na Aishi Manula wapya.

Kauli hiyo imetolewa jijini Dar es Salaam na golikipa wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na Klabu ya Simba, ambaye ni Balozi wa Tecno, Manula, wakati akikabidhi zawadi kwa watoto waliofanya vizuri katika kusakata kabumbu kwenye hitimisho la kampeni ya 'Busti Kipaji'.

„Unakuta mtoto anabidii ya kucheza mpira na hana uwezo wa kununua viatu kwa sababu ni gharama na hali ya Watanzania wa kawaida inajulikana, hivyo niwapongeze Tecno na Airtel kwa kampeni hii ya kusaidia kubusti kipaji cha mtoto mwenye kipaji," alisema Manula.

„Mtoto anapocheza peku bila viatu kuna kuanguka na kuumia na mzazi akiona hivyo anamkataza mwanawe kucheza mpira, lakini hajui kuwa ni vitu vya kawaida hata wachezaji wakubwa tulianza kucheza bila viatu na tumetimiza malengo yetu, hivyo wazazi watoe sapoti kwa watoto wanapoonyesha vipaji vyao," aliongeza.

Alisema kampeni hiyo iliyokuwa inafanywa na Kampuni ya Simu ya Tecno kwa kushirikiana na mtandao wa Airtel, waliandaa bonanza la michezo ambapo wametoa zawadi ya viatu, fedha na jezi kwa washindi ambao ni watoto wasio na uwezo kukimu vifaa hivyo.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa Tecno, Salma Shafi, alisema kuwa kampeni hiyo ilidumu kwa wiki kadhaa na ilianzishwa wakati wa uzinduzi wa simu mpya, Tecno Spack 20 ambapo ilikuwa ukinunua simu moja unamsaidia mtoto mmoja kupata kiatu kimoja.

„Kampeni hii ya Busti Kipaji inayolenga kutoa furaha kwa watoto wenye vipaji imekuwa nzuri ndio maana tumewapa viatu, fedha medali na zawadi mbalimbali kutokana na kufanya vizuri," alisema Salma.

Naye Ofisa Michezo wa Manispaa ya Wilaya ya Ubungo, Wikansia Mwanga, kwa niaba ya mkuu wa wilaya hiyo, alisema amefurahi kuona watoto chini ya miaka 15 wanavipaji vya kutosha, lakini changamoto ni viwanja vya kuchezea.

**KIKAPU...**



Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sabilo kuongoza timu ya 'Beach soccer' COSAFA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Timu ya JKT Tanzania, Sixtus Sabilo, ni mmoja wa wachezaji 26 waliochaguliwa kuunda Timu ya Taifa ya Tanzania ya Soka la Ufukweni kwa ajili ya mashindano ya Afrika Ukanda wa Kusini, COSAFA.

Straika huyo ambaye ndiye tegemeo la JKT Tanzania, amechaguliwa kuwa mmoja wa watakaunda kikosi hicho kwa ajili ya mashindano hayo ya mwaka huu.

Mbali na mchezaji huyo, wachezaji wengine walioteuliwa wanaochezea Ligi Kuu Tanzania Bara ni Ismail Gambo wa KMC na Awadh Salum wa Mtibwa Sugar.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa, amesema ameita kikosi hicho kwa ajili ya kufanya mazoezi na maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo ambayo tarehe ya kuanza na nchi mwenyeji itatangazwa baadaye na wahusika.

Ametangaza wachezaji watakaounda kikosi hicho, mbali na Sabilo kuwa ni Ibrahim Abdallah, Yahaya Tumbo na Juma Sultan kutoka Vingunguti Kwanza, Derick Kanyana na Andrew Daniel (Kijitonyama FC), Haji Ally (KMKM ya Zanzibar), Kelvin Mosha, Jaruph Juma na Goodluck Gama kutoka Friends of Mkwajuni.

Wengine waliochaguliwa ni, Abdulkadir Ally kutoka Zanzibar, Jamal Salehe (Mlandege ya Zanzibar) na Abdulrahim Bausi (Uhamiaji ya Zanzibar).

Beki huyo wa zamani wa Simba na Taifa Stars, pia amewaita kikosini Nicholaus Mbando wa Warriors, Patrick Athanas (Msasani Mabingwa), Adil Nassor (Mburahati FC), Abdilah Mohamed (Ilala FC), Thobias Francis wa Zanzibar, Jume Haji (Kisa FC), Sadiq Salim (Green Warriors) na Mtoro Nassor wa Zanzibar.

## Simba SC na hesabu kali ikiifuata Asec

INATOKA UK. 24

kwa hiyo lilikuwa ni takwa la kiufundi. Tunakwenda kujiandaa na mpinzani mgumu, hivyo lazima upate muda wa kuwaandaa wachezaji.

"Pili ni hatari ya kupata majeraha, katika mechi dhidi ya JKT Tanzania tulipata majeruhi watatu ambao ni Clatous Chama, Sadio Kanoute na Kibu Denis na hiyo ni kutokana na tatizo la ubovu wa uwanja," alisema Benchika kabla ya kuondoka nchini.

Simba itateremka dimbani ikiwa kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa Kundi B, ikiwa na pointi nne, huku Asec Mimosas ikiwa imeshafuzu na pointi zake 10, hivyo inacheza kwa kukamilisha ratiba.

Katika hatua nyingine, Kocha wa makipa wa Simba, Daniel Cadena, ameweka wazi juu ya mabadiliko na kutokuwa na kipa namba moja, kuwa ni kutokana na waliokuwapo ndani ya kikosi cha timu hiyo wameonyesha uwezo mkubwa kila anayepewa nafasi.

Akizungumza na Nipashe jana, Cadena alisema kulingana na ubora wa makipa walionao wamekuwa na wakati mgumu wa kuweza kupata kipa namba moja na kila mmoja amekuwa akipewa nafasi ya kucheza katika mechi tofauti.

Alisema anajivunia kuona makipa wake wanakuwa imara zaidi na kusaidia timu kupata matokeo chanya akiwamo Ayoub, ambaye mechi ya Ligi Kuu iliyopita aliweza kuzuia mashuti mengi kutoka kwa wapinzani wao, JKT Tanzania.

"Ninajivunia kuwa na makipa wazuri na wenye uwezo mkubwa, ukiangalia kiwango cha Manula [Aishi], Hussein [Abel], Ally [Salum] hata Lakred wote wapo vizuri hata mmoja wapo asipokuwapo ndani ya timu kwa changamoto yoyote hatuna presha ya nani kukaa golini," alisema kocha huyo.

## GAMONDI AIFUNGIA KAZI CR BELOUIZDAD

INATOKA UK. 24

kushambulia kwa sababu ya kila mechi tumefanikiwa kufunga bao," alisema Gamondi.

Alisema mechi dhidi ya CR Belouizdad haitakuwa rahisi kwa sababu ya ugumu wa kundi hilo lakini pia baada ya kuwaona wapinzani wake katika mechi na Al Ahly.

"Nimefanikiwa kuangalia mechi yao na Al Ahly, nimeona ubora wao walicheza vizuri na tumeanzia mechi hiyo kufanya maandalizi yetu kuelekea mchezo wetu ujao," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

# Michezo

Jumanne Februari 20, 2024

Nipashe


Ancelotti: Sare yetu sababu si Mbappe UKURASA 21



# SIMBA SC NA HESABU KALI IKIIFUATA ASEC

## ●●●Yabeba majembe 23 bila Ayoub, kocha afunguka sababu kutokuwa na kipa namba moja...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 23 wa Simba kilitarajiwa kuondoka usiku wa manane kuamkia leo kwenda nchini Ivory Coast kwa ajili ya mechi ya raundi ya nne ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas huku Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha akifurahia kupata muda wa kufanya mazoezi na wachezaji wake baada ya kuahirishwa kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar uliokuwa uchezwe juzi, Jumapili.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, kikosi hicho kilitarajiwa kuanza safari saa tisa usiku kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kuelekea Addis Ababa nchini Ethiopia, ambako watakaa kwa saa tatu kabla ya kuunganisha ndege kuelekea jijini Abidjan tayari kwa mechi hiyo itakayochezwa Ijumaa ijayo katika Uwanja wa Felix Houphouet Boigny nchini humo.

Kikosi hicho kinatarajiwa kuwasili Ivory Coast, leo saa 11:00 kwa saa za Afrika Mashariki.

"Tunataraji kusafiri na wachezaji 23 pamoja na watu kadhaa na benchi la ufundi usiku saa tisa tutaanza safari ya kuelekea Adis Ababa Ethiopia, tutakaa pale kwa saa tatu tukisubiri kuunganisha ndege. Tutasafiri pale kwa mwendo usiopungua saa sita na kufika Ivory Coast majira ya saa tisa kwa saa za kule, sawa na saa 11:00 kwa saa za nyumbani Tanzania," alisema Ahmed kabla ya timu hiyo kuanza safari.

Hata hivyo, amesema kikosi hicho kitawakosa wachezaji kadhaa akiwamo kipa tegemeo kwa sasa, Ayoub Lakred, ambaye ana kadi tatu za njano, hivyo kuukosa mchezo huo kikanuni na Willy Onana ambaye anasumbuliwa na nyama za paja.

Ahmed alisema hawana wasiwasi na wanakokwenda kwa sababu wametanguliza watu, wakiongozwa na mratibu Abbas Ally.

"Mechi itakuwa ngumu na kundi ni gumu kwa sababu timu zote tatu, sisi, Jwaneng Galaxy na Wydad Casablanca wote tuna nafasi ya kufuzu," alisema.

Kocha Benchikha kwa upande wake ameonekana kufurahishwa na kuahirishwa kwa mechi dhidi ya Mtibwa ili kupata nafasi ya kuwaandaa vijana wake, baada ya kuikosa kwa siku 15.

"Ni mimi ndiye niliyeomba mechi hii iahirishwe ili kupata nafasi kuwa na vijana wangu kwa ajili ya mazoezi ya jumla, kwani siku zote 15 tulikuwa tunafanya mazoezi kwa ajili ya mechi zilizokuwa zinafululiza,

INAENDELEA UK. 23



Henock Inonga

## Gamondi aifungia kazi CR Belouizdad

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni lazima wapate ushindi wa mabao mengi dhidi ya wapinzani wao, CR Belouizdad ya Algeria utakaochezwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Gamondi amesema baada ya matokeo ya sululu kati ya CR Belouizad na Al Ahly Ijumaa iliyopita nchini Algeria, kundi lao limekuwa gumu na kitu pekee kitakachofanya kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kwenda robo fainali ni ushindi wa mabao mengi, kabla ya kubakisha mechi moja dhidi ya Al Ahly ugenini.


Katika kundi hilo, Yanga inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama tano sawa na CR Belouizdad ambaye ipo nafasi ya pili, Medeama FC ipo nafasi ya nne kwa kukusanya pointi nne na Al Ahly inaongoza kundi hilo ikiwa na alama sita.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema wanafanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huo dhidi ya CR Belouizdad ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa kundi hilo.

Alisema wako kwenye kundi gumu ambalo kila timu ina nafasi ya kwenda hatua ya robo fainali hali ambayo wanatakiwa kupambana na kuumiza kichwa ili kusaka ushindi kwa mechi hiyo ya nyumbani.

"Hakika kila timu inaweza kwenda robo kulingana na kundi lilivyo, tunasahihisha makosa yetu, tumefanikiwa kufanya vizuri kwenye safu ya ulinzi, lakini hata

INAENDELEA UK. 23



Gamondi

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >